epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Ijumaa Oktoba 4, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581819
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22

**MARTÍNEZ: SHANGWE VILLA PARK ZILINIUMIZA MASIKIO**

UKURASA WA 3

**Wanane** mbaroni madai kuhujumu miundombinu gesi

UKURASA WA 19

**Wabunge** Kenya wadai usalama wao uko hatarini



UKURASA WA 19

**Hofu** Israel, Iran kuzidi kuonyeshana umwamba



Gavana wa BoT, Emmanuel Tutuba

# BoT yaondoa hofu uhaba fedha kigeni

UKURASA 2



RIPOTI MAALUM -2

## Gesi yageuka mateso kwa madereva wa magari, bajaji

UKURASA 4




UKURASA 2

Mabaki ya basi lenye namba za usajili T 605 DJR mali ya kampuni ya Kapricon, baada ya kuacha njia na kupinduka katika eneo la Maili Kumi, Korogwe, mkoani Tanga jana, likitokea Dar es Salaam kwenda Arusha na kusababisha vifo vya watu wanne na wengine 15 kujeruhiwa. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

## Wanne walivyofariki dunia, 15 kujeruhiwa katika ajali ya basi

MICHEZO SIMBA SC YAITISHA COASTAL UNION UK.24 KATUNI UK.6

# Wanne walivyofariki katika ajali Korogwe

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

WATU wanne wamefariki dunia na wengine 15 kujeruhiwa, baada ya basi la abiria mali ya Kampuni ya Kapricon Royal Class, kuacha njia na kupinduka katika eneo la Mailikumi, Wilaya ya Korogwe, mkoani Tanga.

Kamanda wa Polisi mkoani humo, Kamishna Msaidizi, Almachius Mchunguzi, alisema ajali ilitokea majira ya saa 7.30 usiku, ikihusisha basi lenye namba T 605 DJR lililokuwa likiendeshwa na Julius Mushi (43), mkazi wa Arusha.

"Tumefuatilia na mpaka sasa waliopoteza maisha ni wanne ambapo wanaume watatu, mwanamke mmoja na wengine 15 wamejeruhiwa, majeruhi wanapatiwa matibabu katika hospitali ya wilaya (Magunga), lakini wengine wamepelekwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Bombo," alisema.

Kamanda Mchunguzi alitoa wito kwa madereva kuwa makini wakati wa kuendesha kwa kufuata sheria za barabarani ili kuzuia vifo na majeruhi ambayo vinaweza kudhibitiwa.

"Wakati wote tunawataka madereva kuchukua tahadhari na kuzingatia sheria za usalama barabarani, udereva ambao unachukua tahadhari wakati wote, wawe makini sana wanapoendesha magari yao.

Kutofuata sheria za barabarani mara nyingi ndio kunasababisha madhara na ajali zinazopoteza maisha ya watu, lakini vilevile tunaweza kupata majeruhi," alisema.

Alipoulizwa kuhusu idadi ya miili iliyopokewa pamoja na majeruhi, Kaimu Mganga Mfawidhi Hospitali ya Korogwe Mji (Magunga), Vasco Lucas, alisema muda wa saa tisa usiku walipokea majeruhi wa basi hilo wapatao 34 ambao kati yao wanaume 19 na wanawake 14 pamoja na watoto wawili wa kiume ambao wamepata majeraha katika sehemu mbalimbali za mwili.

Alisema kati ya majeruhi hao, sita walipatiwa rufani kwa ajili ya matibabu zaidi katika Hospitali ya Rufani ya Bombo, jijini Tanga, lakini pia wamepokea vifo vya watu wanne ambao wamehifadhiwa katika chumba cha kuhifadhia maiti hospitalini hapo.

"Majeruhi waliobaki hospitalini hapa ni 27 ambao wanaendelea na uchunguzi na wengine wameshatibiwa na kuruhusiwa baada ya hali zao kuendelea vizuri huku idadi yao ikizidi kupungua," alisema.




Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Emmanuel Tutuba (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu asilimia sita ya riba ya BoT. Kushoto ni Naibu Gavana Sera za Uchumi na Fedha, Dk. Yamungu Kayandabila na Mkurugenzi wa Utafiti na Sera za Uchumi, Dk. Suleiman Missango. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# BoT yaondoa hofu uhaba fedha za kigeni

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imewaonmdoa hofu wananchi kuhusu upatikanaji wa fedha za kigeni huku ikisema umeimarika katika kipindi cha Julai hadi Septemba, mwaka huu.

Imesema kuimarika huko kulikwenda sambamba na msimu wa shughuli za utalii na mauzo ya mazao ya kilimo na biashara nje ya nchi.

Gavana wa BoT, Emmanuel Tutuba, alisema jana jijini hapa kuwa kutokana na mwenendo huo, kasi ya kuporomoka kwa thamani ya shilingi ilipungua hadi kufikia asilimia 10.1 kwa mwaka unaoishia Septemba 2024, kutoka asilimia 12.5 kwa mwaka ulioshia Juni 2024,"alisema.

Alibainisha kuwa akiba ya fedha za kigeni iliongezeka kufikia dola za Marekani milioni 5,413.6 mwishoni mwa Septemba kutoka dola za Marekani milioni 5,345.5 Juni, mwaka huu na kwamba kiasi hicho kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi kwa zaidi ya miezi minne.

Tutuba alisema hali hiyo inatarajiwa kuimarika kutokana na ongezeko la bei ya dhahabu kwenye soko la dunia, shughuli za utalii na mauzo ya bidhaa asilia kama korosho, tumbaku, kahawa na pamba.

Pia alisema mauzo ya mazao ya chakula hususan mahindi na mchele kwenda nchi jirani, pia yanatarajiwa kuongeza mapato ya fedha za kigeni.

"Kupungua kwa uagizaji wa mbolea na kupungua kwa bei za bidhaa za mafuta ya nishati kunatarajiwa kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni na matakwa ya kisheria kuhusu kunukuu na kufanya malipo ya ndani kwa shilingi ya Tanzania yanatarajiwa kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni nchini na kuongeza ufanisi wa sera ya fedha," alisema.

Alisema mpango wa ununuzi wa dhahabu katika soko la ndani kwa kutumia Shilingi ya Tanzania utaongeza akiba ya fedha za kigeni.

RIBA YA BENKI

Gavana Tutuba alisema Kamati ya ya Sera ya Fedha ya BoT imeamua riba ya benki ya asilimia sita iliyodumu kuanzia Aprili mwaka huu iendelee kwa robo mwaka itakayoishia Desemba, mwaka huu.

Aidha, alisema sababu zilizochangia riba ya Benki Kuu (CBR) kwa robo ya mwisho ya mwaka 2024 kubaki asilimia sita kuwa ni pamoja na kukua kwa uchumi nchini na duniani huku ikitarajiwa kuwapo na ongezeko la upatikanaji wa fedha za kigeni.

"Uamuzi huu ulitokana na matarajio ya mfumuko wa bei kuendelea kuwa chini ya lengo la nchi la asilimia tano. Kamati pia inatarajia uchumi kuendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha, sambamba na kuimarika kwa mazingira ya kiuchumi duniani na hapa nchini," alisema.

Alisema uchumi wa dunia unatarajiwa kuendelea kukua sambamba na kuimarika kwa mazingira ya upatikanaji fedha na kutokana na hali hiyo, Shirika la Fedha Duniani (IMF) na Benki ya Dunia wanakadiria uchumi wa dunia kukua kwa asilimia 3.2 na asilimia 2.6, mtawalia mwaka 2024.

Mwenendo huo, alisema unatarajiwa kuchagiza shughuli za uzalishaji hapa nchini na Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kupungua, ikiwa ni matokeo ya utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kupunguza ongezeko la ukwasi sambamba na kupungua kwa bei za bidhaa katika soko la dunia, husuan mafuta na mbolea.

"Katika robo ya mwaka inayoishia Desemba 2024, bei za mafuta ghafi zinatarajiwa kuwa kati ya dola za Marekani 72 hadi 82 kwa pipa, kutokana na ongezeko la uzalishaji. Hali hii inatarajiwa kupunguza ongezeko la mfumuko wa bei na mahitaji ya fedha za kigeni nchini kwa kuwa bidhaa za mafuta huchangia takriban asilimia 20 ya bidhaa zote zinazoagizwa kutoka nje ya nchi," alisema.

**KUKUA UCHUMI**

Tutuba alisema katika robo ya kwanza ya mwaka 2024, uchumi ulikua kwa asilimia 5.6, huku shughuli za ujenzi, kilimo, fedha na bima, na usafirishaji zikichangia kwa kiwango kikubwa katika ukuaji huu.

"Kwa mujibu wa viashiria vya awali, uchumi unakadiriwa kukua kwa asilimia 5.8 na asilimia 5.6 katika robo ya pili na ya tatu ya mwaka 2024, mtawalia na unatarajiwa kuendelea kukua katika viwango hivyo katika robo ya mwisho wa mwaka,"alisema Tutuba.

Hata hivyo, alisema kuendelea kuimarika kwa mazingira ya kiuchumi nchini kunatokana na maboresho katika biashara na uwekezaji, ikiwamo yanayoendelea kutekelezwa kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo.

"Uzalishaji katika shughuli za kilimo unatarajiwa kuongezeka kwa kiwango kikubwa kutokana na matumizi ya pembejeo (mbolea na mbegu bora), viwatilifu na uwekezaji katika miradi ya umwagiliaji. shughuli za ujenzi na usafirishaji zinatarajiwa kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi,"alisema.

MIKOPO CHECHEFU

Gavana Tutuba alisema mikopo kwa sekta binafsi imeendelea kuongezeka kwa kasi ya kuridhisha ikiwa ni takriban asilimia 17.1 kwa kipindi cha Julai hadi Septemba 2024 na ubora wa rasilimali za benki umeongezeka ambapo uwiano wa mikopo chechefu ulipungua hadi asilimia 3.9 mwezi Agosti 2024, kutoka asilimia 5.1 katika mwezi kama huo mwaka 2023.

**DENI LA TAIFA**

Alisema Deni la Taifa limefikia dola za Marekani milioni 37,721.6, sawa na asilimia 46.9 ya Pato la Taifa (GDP), ambalo ni chini ya kigezo cha mtangamano wa kiuchumi cha ukomo wa asilimia 60 kwa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Aidha, alisema uwiano wa deni kwa Pato la Taifa, kwa thamani halisi ya sasa (NPV) ulikuwa asilimia 36.4 mwaka 2023/24, chini ya kigezo cha mtangamano wa kiuchumi cha ukomo wa asilimia 50 kwa EAC.

Pia alisema kupungua kwa athari za mitikisiko ya kiuchumi duniani nakisi ya urari wa malipo ya kawaida inakadiriwa kupungua hadi kufikia asilimia 3.2 kutoka 4.4 kwa kipindi kama hicho mwaka 2023.

"Mwenendo huu ulitokana na ongezeko la mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi, hususan utalii, dhahabu, tumbaku na korosho. Nakisi ya urari wa malipo ya kawaida inatarajiwa kuendelea kuimarika na hivyo kusaidia kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni nchini,"alisema.

# Theluthi ya watoto nchini wana udumavu

**Na Vitus Audax**, MWANZA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema licha ya juhudi zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau kutoka sekta binafsi na kimataifa, theluthi moja ya watoto nchini wana udumavu.

Majaliwa alisema hayo jana mkoani hapa wakati akifunga Mkutano Mkuu wa 10 wa Wadau wa Lishe nchini huku akibainisha kuwa takwimu zilizotolewa na Tanzania Demographic Health Survey (TDHS) mwaka 2018, zinaonesha theluthi moja ya watoto wamedumaa.

Alisema licha ya tatizo hilo bado kuna ongezeko la magonjwa sugu yasiyoambukiza yanayotokana na lishe duni na kuwataka wadau kuongeza nguvu katika kutekeleza malengo ya afua ya lishe.

Majaliwa alisema kutokana na tatizo hilo, kuna umuhimu wa wadau mbalimbali kuandaa mjadala mpana wa kitaifa ili kuleta msisitizo katika utekelezaji wa mipango ambayo tayari imewekwa na serikali pamoja na wadau.

Aliagiza kutolewa kwa elimu na msisitizo kuhusu lishe katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuifanya kuwa ajenda ya kitaifa katika nyumba za ibada pamoja na kwenye vyombo vya habari.

"Juhudi za serikali zinaendelea zikiongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan kusainisha mikataba wakuu wote wa mikoa kuhakikisha wanatekeleza afua hiyo.

"Niagize TAMISEMI (Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa) kuhakikisha inasimamia kwa ukamilifu mikataba hiyo itekelezwe," alisema.

Majaliwa aliwataka wadau wa maendeleo likiwamo Shirika la GAIN Tanzania pamoja na SANKU kuimarisha utekelezaji wa programu ya uongezaji wa virutubishi kwenye vyakula hususani maeneo ya vijijini.

"Lengo ni kuhakikisha nchi inakuwa na uhakika wa uwapo wa mashine za bei nafuu za kuchanganyia virutubishi na upatikanaji wa virutubishi vinavyozalishwa kwa kutumia malighafi inayopatikana ndani ya nchi kwa bei nafuu," alisema Majaliwa.

Akitoa tathmini ya mkutano huo Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Dk. Jim Yonazi, alisema zaidi ya watoto milioni tatu nchini wana tatizo la udumavu, hali aliyoitaja kuwa mbaya zaidi kwa taifa la baadaye.

Dk. Yonazi alisema zaidi ya watoto 600,000 wana utapiamlo mkali sambamba na ukondefu wa asilimia 3.5 kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2015.

Alisema kutokana na hali hiyo, mkutano huo umetoka na maazimio matano ili kukabiliana na lishe duni kwa watoto ikiwa ni pamoja na masuala ya huduma ya lishe yajumuishwe katika Dira ya Taifa 2050.

Meneja wa Mradi, Programu ya Uimarishaji Chakula kutoka Shirika la GAIN Tanzania, Archard Ngemela, alisema ili kukabiliana na udumavu nchini, kuna uhitaji mkubwa wa jamii kupata unga uliorutubishwa.

Alisema katika kuisaidia jamii kupata unga wenye virutubisho, shirika hilo limekuja na mradi wa mashine yenye uwezo kusindika unga kwa kuchanganya virutubisho muhimu ikiwa na lengo la kuzisaidia shule kupata huduma hiyo muhimu.

"Wazazi wamekuwa wakichanga mahindi shuleni kwa ajili ya chakula cha Watoto, lakini wamekuwa hawapati unga uliorutubishwa, hivyo kufanya hali ya udumavu kwa watoto kuendelea kuwa kubwa nchini," alisema.

Ngemela alisema mashine hiyo imetengenezwa nchini na wadau wa PEC ikiwa na uwezo wa kutumia umeme wa nishati jua ili kumudu hali ya mazingira ya watu wasiyo kuwa na umeme.

Meneja Mradi wa Afya na Lishe kwa Kuzingatia Usawa wa Kijinsia kutoka Shirika la World Vision Tanzania, Shukrani Dickson, alisema bado jamii imeshika mila na desturi potofu zinazodidimiza mwanamke na kumfanya mwanamume kuwa na uamuzi wa kipi kitaliwa nyumbani na kwa nini.

Dickson alisema kukabiliana na hali hiyo iliyobainika katika mikoa ya Simiyu na Shinyanga, shirika hilo limeanza kumshirikisha kwa karibu mwanamume katika afua za lishe ili kuondoa ule utamaduni wa kuuza mazao na vitu muhimu vyenye lishe kisha kuiacha familia na chakula cha aina moja.

"Kupitia modo yetu ya 'men care' tunahakikisha tunatoa elimu kwa jamii hasa kwa wanaume, kujua umuhimu wa vyakula vya asili kama vile mayai, kuku, choroko na vingine ambavyo mara nyingi wamekuwa wakiviuza na kuiachia familia mahindi pekee," alisema.

# Wanane mbaroni kwa madai kuharibu miundombinu ya gesi

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linawashikilia watu 11, wakiwamo wanane wanaotuhuma kwa uharibifu wa miundombinu ya bomba la gesi la ORYX linalosafirisha nishati hiyo kutoka Bandari ya Dar es Salaam.

Wengine watatu wanatuhumiwa kwa wizi wa madini aina ya Cooper Cathode yaliyokuwa yakisafirishwa kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kwenda Bandari ya Dar es Salaam.

Kamanda wa Kanda hiyo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Aliwataja wanaoshikiliwa tuhuma za kuhujumu bomba la mafuta ni Twaha Salum (53) na wenzake saba.

"Watuhumiwa hawa wamehojiwa kwa kina na ushahidi umekusanywa na watafikishwa kwenye mamlaka zingine kwa hatua zaidi za kisheria," alisema.

Kuhusu wanaotuhumiwa kuiba madini, Kamanda Muliro alisema, wanamshikilia Daudi Matola (50), ambaye ni dereva mkazi wa Kimara, wilayani Kinondoni, mkoani humo, na wenzake wawili kwa tuhuma zao.

Alisema tukio hilo lilitokea Agosti 7, mwaka huu, wakati dereva huyo na wenzake wawili wakiwa na gari T 882 DQK aina ya Benz na tela T 884 EEE mali ya Kampuni ya FAA Trucks, ambao baadaye walilitelekeza Dar es Salaam.

Kutokana na tukio hilo, Kamanda Muliro alitoa wito kwa wananchi kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kutoa taarifa na kuahidi kutokuwa na huruma kwa wahalifu na kuendela kuwashughulikia vikali kwa mujibu wa sheria.




Watu 11 wanaotuhumiwa kwa makosa mbalimbali likiwamo la kuhujumu miundombinu ya mabomba ya gesi ya Kampuni ya Oryxy na kukutwa na madini ya shaba, wakiwa chini ya ulinzi, wakati wakishuka kwenye gari baada ya kufikishwa katika Kituo cha Polisi Kati, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# TEF yashtushwa kufungiwa mitandao kijamii Mwananchi

**Na Romana Mallya**

JUKWAA la Wahariri Tanzania (TEF) limeshtushwa na taarifa za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kusitisha kwa siku 30 leseni za huduma za maudhui mtandaoni za Kampuni ya Mwananchi Communications Limited.

Kampuni hiyo inamiliki magazeti ya The Citizen, Mwananchi na MwanaSpoti pamoja na Mwananchi Digital.

Taarifa iliyotolewa juzi na Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, ilisema kampuni hiyo ilichapisha maudhui yaliyokiuka kanuni ambayo yameleta tafsiri hasi kwa taifa, jambo ambalo linaathiri na kuharibu umoja, amani na mshikamano wa kitaifa.

Mwenyekiti wa TEF, Deodatus Balile, alisema jana kuwa: "Kwa muda mrefu TEF tumekuwa tunalalamikia mamlaka makubwa yanayotolewa kisheria kwenye taasisi au wakuu wa taasisi ya kuwa walalamikaji, waendeshaji mashtaka na watoa hukumu bila upande wa pili unaotuhumiwa kupewa fursa ya kusikilizwa wazi hadharani.

"Tutaendelea kudai haki hii ya asili (natural justice) ya chombo cha habari kinachotuhumiwa kupewa hati ya mashtaka, kikajitetea mbele ya taasisi huru au mahakama, kisha uamuzi ufanyike ambao ndiyo utawala wa sheria, badala ya sasa ambapo sheria inatoa mamlaka kwa mtu mmoja kufanya uamuzi mzito kama huu."

Balile alisema kampuni ya Mwananchi walipaswa kufunguliwa mashtaka katika chombo huru na wao kujitetea kisha chombo hicho kutoa hukumu kulingana na mashtaka yaliyowasilishwa mbele yake.

"Tumeviona pia vibonzo au maudhui yaliyolalamikiwa na TCRA. Tunawasihi wahariri na watendaji wa vyombo vya habari kufahamu kuwa sheria mbaya inaendelea kuwa sheria hadi itakapobadilishwa.

"Tunawasihi wahariri na waandishi nchini kufahamu ukweli kuwa utamaduni unatofautiana nchi hadi nchi na zipo njia za kufikisha ujumbe kwa njia sahihi, badala ya kujiingiza katika mazingira yanayoweza kutafsiriwa kama kejeli," alisema.

Balile alisema kwa vyovyote vile, tayari tatizo limetokea na kinachotakiwa sasa ni kushauri pande zote mbili; serikali na Mwananchi Communications wakutane na kujadili suala hilo na kulimaliza kwa maslahi mapana ya taifa na uhuru wa vyombo vya habari ndani ya muda mfupi kadri inavyowezekana.

RIPOTI MAALUM -2

# Gesi yageuka mateso kwa madereva magari na bajaji

Na Halfani Chusi

**HII ni sehemu ya pili ya ripoti inayoangazia madhila wanayopata madereva wa vyombo vya moto vinavyotumia gesi mkoani Dar es Salaam.**

**Katika sehemu ya kwanza jana, kulikuwa na ushuhuda wa adha wanazopata madereva hao, hata kukaa kwenye foleni ya kujaza gesi kwa saa nane. Endelea...**



Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Immaculate Semes



Naibu waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko

KAIMU Mkurugenzi wa Biashara ya Gesi na Mafuta wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Emmanuel Gilbert, anasema mkakati uliopo unajumuisha ujenzi wa vituo vingine vidogo mkoani Morogoro na vingine viwili mkoani Dodoma, ambavyo vitakamilika ndani ya miezi sita hadi saba kuanzia mwezi uliopita.

Anasema kuwa kwa sasa tayari kuna kampuni 31 ambazo zimeshapata kibali kutoka TPDC na ziko kwenye hatua mbalimbali za kupata ridhaa kutoka kwa msimamizi wa sekta.

Anasema baada ya kuwapatia idhini ya kuwekeza, wanakwenda Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kupitishwa katika mchakato wa ujenzi ili vituo vijengwe kwa usalama na viwango vinavyotakiwa.

"Kuna kampuni kadhaa ziko kwenye mchakato huo, ndani ya mwaka 2024/25 tunategemea kuwa na vituo vipya 14, ukiachana na hivi vilivyopo. Kati ya vituo hivyo 14, vya TPDC vitakuwa saba na vingine ni kutoka kampuni binafsi.

"Kwa mwaka 2025/26 tunategemea kuwa na vituo 14 tena. Kati yake, vitano vitakuwa vya TPDC na tisa vya kampuni binafsi. Mwaka 2026/27, kutakuwa na vituo vingine 19. Kati yake, vinane vitakuwa vya TPDC na vingine vitakuwa vya kampuni binafsi.

"Kwa hiyo, unaweza ukaona mwanga umeanza kuonekana, uwekezaji kwenye gesi asilia kwa ajili ya magari ni huduma inayopanuka na inaweza kuja kuwa kubwa kuliko ya mafuta. Gesi inauzwa bei rahisi kuliko mafuta," Gilbert anasema.

Ofisa huyo wa TPDC anasema lengo la serikali ni kuhakikisha itakapofika 2030, mwaka ambao ni ukomo wa upimaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu, walau asilimia 80 ya Watanzania wote wenye vyombo vya moto wawe wanatumia nishati safi kuendesha vyombo vyao.

"Gesi ni fursa, gharama ya ununuzi wa mafuta kwa sasa lita moja ni Sh. 3,300 wakati bei ya gesi kilo moja inauzwa Sh. 1,550. Matumizi ya gesi pia yanasaidia kutunza mazingira kwa sababu gesi haitoi moshi," anasema.

Gilbert anasema baadhi ya nchi zimepiga marufuku matumizi ya vyombo vya moto vinavyotumia mafuta, akitolea mfano magari ya kusambaza bidhaa kwenye maduka mijini, magari ya wanafunzi na taxi.

"Wote hao wanalazimishwa kama hawatumii gesi asilia, hawawezi kupata kibali, hivyo na sisi tunafikiria tutafika huko tutakapokuwa tumepata vituo vingi vya kutoa huduma. Hivi sasa tukiweka masharti hayo, maana yake tutaua ajira hizo," Gilbert anahitimisha ufafanuzi wake.

Kukabiliana na uhaba wa vituo vya kujaza gesi nchini, Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa EWURA, Titus Kaguo, anasema yamefanyika marekebisho ya sheria, wakitoa rukhsa vituo vyote vya mafuta zaidi ya 2,000 nchini vinaweza kuwekwa huduma ya kujaza gesi.

Anasema taratibu za kisheria zimerekebishwa ili kuwezesha kituo cha mafuta kuwa na miundombinu ya gesi, akibainisha kuwa tayari wamepokea maombi ya kampuni zinazotaka kuwa na huduma hiyo katika vituo vyake vya mafuta.

Kaguo anasema vigezo vya kufungua kituo cha kuuzia gesi, ni sawa na vinavyotumika kufungua kituo cha mafuta huku akiunga mkono hoja kwamba, vituo hivyo vikitapakaa nchi nzima, vitasaidia kufikia adhima ya kupunguza uchafuzi wa mazingira kupitia nishati chafu.

Changamoto ya uhaba wa vituo vya gesi inafahamika kwa Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Felchesmi Mramba. Anawatoa hofu watumiaji wa nishati hiyo kwamba serikali inafanyia kazi suala hilo.

Anasema upatikanaji wa uhakika wa gesi asilia kwa ajili ya vyombo vya moto utawarahisishia wafanyabiashara na wakulima usafirishaji mizigo yao kwa gharama ndogo na kupata faida kubwa.

Watafiti wanabainisha kuwa moshi unaotolewa na magari una hewa ya kaboni monoksaidi, nitrojeni oksaidi na kemikali nyinginezo ambazo zimethibitishwa kusababisha maradhi mbalimbali, ikiwamo saratani.

Ripoti iliyotolewa Februari mwaka huu na Baraza la Kimataifa la Usafiri Salama (ICCT) inaonesha kuwa watu 385,000 walifariki dunia kutokana na moshi unaotolewa na magari kote duniani mnamo mwaka 2015.

Ripoti hiyo inafafanua zaidi kwamba magari yanayotumia dizeli yalichangia zaidi vifo hivyo, yakitajwa kuchangia asilimia 66 ya madhara hayo.

Watafiti hao wanataja mataifa ya Ufaransa, Ujerumani, Italia na India kuwa na magari mengi yanayotumia dizeli, wakibainisha kuwa sekta ya usafiri huchangia asilimia 11 ya vifo vyote vinavyotokana na hewa chafu duniani.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, watu 114,000 walifariki dunia China kutokana na moshi unaotokana na magari mnamo mwaka 2015 huku watu 22,000 wakiaga dunia Marekani kutokana na tatizo hilo.

Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Immaculate Semesi, anasema uhaba wa vituo vya kujazia gesi ni kikwazo katika kufikia adhima ya kuwa na mazingira safi nchini.

"Ule moshi unaotokana na vyombo vya moto hutengeneza kitu kama blanketi fulani angani, matokeo yake ndio huwa unaona kuna wakati kuna joto la kupitiliza, mvua za kupitiliza au ukame.

"Mabadiliko ya namna hiyo ndio yanasababisha madhara kwa mazingira na binadamu wakati mwingine yanaathiri afya kwa kuzalisha mbu wengi, magonjwa ya mlipuko, kukosekana kwa malisho, mafuriko, mmomonyoko wa udongo na mavuno hafifu kwa sababu mabadiliko ya tabianchi huja na mambo mengi," anasema.

Kwa kuzingatia madhara hayo, mkurugenzi huyo anasema kuwa mara zote wamekuwa wanahimiza wamiliki wa vyombo vya moto kutumia gesi asilia ili kupunguza athari za kimazingira.

Dk. Immaculate, akieleza kuvutiwa na mwamko wa wananchi kutumia gesi katika vyombo vya moto, anashauri serikali na sekta binafsi kuweka nguvu ya pamoja kuongeza vituo vya gesi ili kupunguza msongamano wa magari na bajaji kwenye vituo vichache vya kujazia gesi vilivyoko.

Kero ya uhaba wa vituo vya gesi ilishafikishwa mezani kwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko ambaye hatua za awali alizochukua ni pamoja na kuitaka EWURA kuwezesha ujenzi wa vituo vingi zaidi nchini.

"Tujenge vituo vingi hapa Dar es Salaam, magari ya mafuta ni mengi sana, tukipunguza hiyo volume (kiwango) ya mafuta, magari yakatumia gesi, gharama ya uendeshaji hayo magari itapungua.

"Huu ni mpango wa muda mrefu ambao tutaendelea kuwa nao. EWURA lazima wauchukue kwa kasi kubwa ili utupe matokeo mazuri," anaagiza Dk. Biteko.

Wakati wa Mkutano wa 11 wa Wawakilishi wa Kudumu wa Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP) jijini Nairobi, Kenya Julai mwaka huu, wawakilishi Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi walikubaliana nchi zao kutunga sheria zitakazohakikisha magari yanayoingizwa ukanda wa Afrika Mashariki yana teknolojia inayosafisha moshi.

# Mpango ataka mabunge Afrika kutilia mkazo kilimo

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ameyataka mabunge barani Afrika kuwekeza nguvu zaidi katika kuimarisha uwekezaji wa umma kwenye sekta ya kilimo ili kutafuta suluhu ya matatizo ya vijana.

Pia ameyataka kushirikiana na serikali zao katika kubuni na kufadhili ubunifu wa vijana katika kuondokana na tatizo kubwa la uhaba wa ajira linalowakabili vijana barani.

Dk. Mpango alieleza hayo jana jijini Arusha alipofungua mkutano mkuu wa mwaka wa 53 wa Mabunge Wanachama wa Nchi za Jumuiya ya Madola Kanda ya Afrika (CPA-AFRICA), akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema ni muhimu wabunge kukuza sera na programu zinazounga mkono ajira, ufadhili wa kibunifu, kutetea maboresho ya sekta ya elimu na mafunzo pamoja na matumizi ya teknolojia kwenye sekta mbalimbali kama sehemu ya kuondokana na tatizo la ajira kwa vijana wa barani Afrika.

Kabla ya ufunguzi huo, Spika wa Bunge la Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Dk. Tulia Ackson, alimweleza Makamu wa Rais kuwa mkutano huo unaangazia masuala ya usalama wa chakula, mabadiliko ya tabianchi na changamoto ya ajira kwa vijana.

Alisema katika masuala ya chakula, wabunge kupitia CPA AFRIKA, kila nchi inatoa mtazamo wake katika usalama wa chakula, lakini upande Tanzania, iko tayari kuwaonesha jinsi gani wanavyopambana katika suala la kilimo ingawa nchi za Afrika zinakabiliwa na changamoto za ukosefu wa chakula.

Alisema katika kuonesha jinsi Tanzania inavyopambana na suala la kilimo, washiriki hao watatembelea wilayani Arumeru kujionea mashamba ya mfano ya vijana wanaojihusisha na kilimo, ukiwamo utunzaji mazingira katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Spika Tulia pia alimpongeza Rais Samia kwa kuwa kinara wa kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia, akilitaja ni eneo lingine kwa vijana kupata ajira.

Spika wa Bunge la Malawi ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati Tendaji ya CPA - AFRIKA, Catherine Hara, alisema nchi za Afrika bado ziaendelea kukabiliana na changamoto ingawa zinaendelea kushughulikiwa ili kukuza uchumi, ukiwamo uhaba wa chakula, unaotokana na mabadiliko ya hali ya hewa.

"Mabunge lazima yawe mstari wa mbele katika sera zinazohakikisha kunakuwa na mikakati ya kilimo endelevu, maendeleo ya mifumo ya chakula cha kustahimili mabadiliko, njaa na utapiamlo.

Spika wa Bunge la Sierra Leone, ambaye ni Rais wa CPA - AFRIKA, Segepoh Solomon, alimpongeza Rais Samia kwa kukuza demokrasia, utawala bora na kuinua uchumi wa nchi na wananchi.

# Mchengerwa aagiza kuangaliwa vigezo Mji Mdogo Ngaramtoni uwe Halmashauri

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, amemwagiza Katibu Tawala Mkoa wa Arusha, Missaile Mussa kushirikiana na viongozi wa Halmashauri ya Arusha kupitia na kuangalia kama Mamlaka ya Mji Mdogo wa Ngaramtoni imekidhi vigezo ili ipandishwe hadhi ya kuwa Halmashauri ya Mji.

Ameelekeza mchakato uanzie ngazi ya wilaya na upelekwe Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) na kisha upelekwe Ofisi ya Rais - TAMISEMI na endapo watajiridhisha kuwa wamekidhi vigezo, watamwandikia Rais Samia Suluhu Hassan ombi la ridhaa ya kupandishwa hadhi.

Waziri Mchengerwa aliagiza hayo jana wakati wa ziara yake katika Halmashauri ya Arusha, wilayani Arumeru, mkoani Arusha ambako alikagua miradi ya maendeleo.

Alisema endapo mchakato huo ukikamilika, wauwasilishe TAMISEMI waupitie na baadaye wataomba ridhaa kwa Rais.

"Anzeni mchakato wa kupitia vigezo vyote vilivyowekwa na kama kuna mahali utaona kuna uhitaji zaidi, wasilianeni na TAMISEMI ili tumwandikie Rais na jambo hili lianze mara moja," aliagiza.

Waziri huyo alisema kuwa endapo mji mdogo huo ukipandishwa hadhi na kuwa Halmashauri ya Mji, utasaidia kuleta chachu ya maendeleo na kukua kwa kasi zaidi kiuchumi.

Alisema mamlaka hiyo ya mji mdogo ikitolewa na kuwa Halmashauri ya Mji, itawezesha halmashauri hiyo kujikwamua kiuchumi na kupata maendeleo zaidi kwa kuwa mji mdogo unakuwa na matumizi makubwa ya fedha, hivyo wanajikuta wanashindwa kufanya mambo ya maendeleo.

Alisema Rais Samia amedhamiria kuhakikisha anakuza na kuimarisha mamlaka za kiutawala ili wananchi wanufaike na huduma karibu na serikali.

"Katibu Tawala Mkoa na wilaya mchakato uanzie wilayani, uletwe mkoani kwa ajili ya kuchakata hoja za kuanzishwa kwa Halmashauri ya Mji kutoka Mamlaka ya Mji Mdogo kisha uwasilishwe kwetu," alisisitiza.

Kuhusu suala la mji mdogo Waziri Mchengerwa, alisema dhamira ya Rais Samiani kupandisha hadhi vitongoji kuwa vijiji na vijiji kuwa miji, hivyo Mamlaka ya Mji Mdogo Ngaramtoni inaweza kupandishwa hadhi.

Alisema serikali imetoa fedha nyingi katika Shule ya Sekondari Kiutu pamoja na Hospitali ya Wilaya - Olturumeti ambayo ni moja ya hospitali ambazo serikali imetoa fedha nyingi kwa ajili ya ukarabati kwa kuwa ni miongoni mwa hospitali 129 nchini zilizokarabatiwa. Kati yake, hospitali 50 ni kongwe.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, aliseme mkoa huo hauongozwi na mtu mmoja, bali viongozi wote, wakiwamo madiwani na wenyeviti wa mitaa, vijiji na vitongoji, hivyo wanapaswa kushirikiana pamoja kuleta maendeleo.


## HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

## TANGAZO LA MRADI WA VIWANJA ENEO LA KIKOMBO KITALU "DA" NA "N"

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE AMBAO HAWAJAKAMILISHA MALIPO YA UNUNUZI WA VIWANJA KATIKA MRADI WA VIWANJA ENEO LA KIKOMBO KATIKA KITALU "DA" NA "N" KUWA WANATAKIWA KUKAMILISHA MALIPO YOTE NDANI YA SIKU KUMI NA NNE (14) KUANZIA TAREHE 3 HADI 16 OKTOBA, 2024.

KUSHINDWA KUKAMILISHA MALIPO HAYO; KIWANJA HICHO KITATOLEWA KWA MWOMBAJI MWINGINE BILA TAARIFA ZAIDI KWAKO NA WEWE UTAREJESHEWA FEDHA YAKO BAADA YA KUKATWA ASILIMIA 10 KWA GHARAMA ZA USUMBUFU.

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA MKURUGENZI WA JIJI LA DODOMA**



## TANGAZO LA NOTISI YA KULIPA DENI LA MKOPO

Tujijenge Tanzania Financial Services Ltd, inatangaza notisi ya siku kumi na nne (siku 14) kwa wadaiwa waliyochukua mikopo na kushindwa kulipa kulingana na makubaliano na masharti ya mikopo yao. Endapo kama watashindwa kulipa madeni yao kulingana na muda ulioainishwa kwenye tangazo hili gazetini, taratibu zingine za kisheria zitachukuliwa dhidi yao ikiwa ni pamoja na kuwaruhusu madalali kukamata na kuuza mali walizoweka dhamana ya mikopo yao

| | JINA LA MTEJA | MKOA | | JINA LA MTEJA | MKOA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | UWESU ATHUMANI MACHO | | | | |
| 2 | KASSIM SHABANI MORY | DSM | 41 | GRACE MATHIAS KOMBO | DSM |
| 3 | MUZAMILY OMARY SEMKONDO | DSM | 42 | JULIANA JACKSON MUHILA | DSM |
| 4 | IMAM SADIKI SHEKULAMBA | DSM | 43 | AMINA ISSA JUMA | DSM |
| 5 | ZUHURA EDWINI MWASONGWE | DSM | 44 | ASHURA SALUM ALLY | DSM |
| 6 | JOYCE PONSIAN KATULA | DSM | 45 | REHEMA MFAUME ALLY | DSM |
| 7 | AGNES MOHAMED ALI | DSM | 46 | ZAITUNI SAIDI MCHONGELA | DSM |
| 8 | ALLY BENITHO MWAKITOSI | DSM | 47 | MARIA YOTAM MAHEMELO | DSM |
| 9 | ALLY HASSAN GODA | DSM | 48 | ROSE CHARLES JOHN | DSM |
| 10 | SIKUDHANI SHOMARI WAZIRI | DSM | 49 | ANNA PAULO MROSSO | DSM |
| 11 | JAMES ALOYCE KOMBA | DSM | 50 | ZENA JAMALI RIDHIWANI | DSM |
| 12 | SAIDI RASHIDI MALIKA | DSM | 51 | DEBORA ELIA MWEGOHA | DSM |
| 13 | MOHAMED ALLY JUMA | DSM | 52 | TINA STIVINI NZALLAH | DSM |
| 14 | JEROME P KILIMBIDA | DSM | 53 | AMINA BUSHIRI MBAMBA | DSM |
| 15 | RAJABU OMARY MANDA | DSM | 54 | ZIADA SAID MAKAKALA | DSM |
| 16 | ASHA MOHAMED SAID | DSM | 55 | REHEMA ATHUMANI IBRAHIM | DSM |
| 17 | MFAUME ALLY BWAMKUU | DSM | 56 | KHADIJA MOHAMEDI SALUM | DSM |
| 18 | BETHOD IGNAS MDEKE | DSM | 57 | MMANGA SALUM SLEYOUM | DSM |
| 19 | JAMES COSMAS MFALAMAGOHA | DSM | 58 | HAIRUN LEONARD MACHA | DSM |
| 20 | MTWENYA MAYUNGA MATOFAL | DSM | 59 | SARAFINA PATRICK MADELEKE | DSM |
| 21 | MASHAKA SELEMANI POLI | DSM | 60 | AZMMIINAH KAREEM MSHAHARA | DSM |
| 22 | OMARI SAID MWANGU | DSM | 61 | ELIZABETH MICHAEL CHIN'GOLA | DSM |
| 23 | MASHA TWAHA YASIN | DSM | 62 | SUZAN YOHANA CHILUNDA | DSM |
| 24 | EMELDA KIVUMBI LWENA | DSM | 63 | LEAH EDWIN LENDO | DSM |
| 25 | SAMSON ABRAHAM LUKINGA | DSM | 64 | JOHARI SHABANI JUMA | DSM |
| 26 | HAMISI ABDALLAH OMARY | DSM | 65 | FATUMA RAMADHANI MCHIMA | DSM |
| 27 | JERADINA MARKO SONYO | DSM | 66 | KHADIJA TAMBWE ABDALLAH | DSM |
| 28 | BRENDA AMEDEUS MSENGI | DSM | 67 | MOHAMED CLAUDIO KILAGA | DSM |
| 29 | JAMILA LEVI JOSEPH | DSM | 68 | FLORA FIDELIS TINZARA | DSM |
| 30 | FATUMA ISSA ABED | DSM | 69 | MWAMVITA MOHAMMEDI SALUM | DSM |
| 31 | ANNA ABINER MALISA | DSM | 70 | WINFRIDA EMMANUEL NGAHALA | DSM |
| 32 | ALLEN HUMPHREY MLATI | DSM | 71 | MESHACK ENOCK LUENA | DSM |
| 33 | JANE WILLIAM SHUMA | DSM | 72 | MAUA MOHAMEDI ATHUMAN | DSM |
| 34 | BARAKA JAMESI MWAIKAMBO | DSM | 73 | ASHA SAIDI MANYIMANYI | DSM |
| 35 | TAUSI JUMA RAMADHANI | DSM | 74 | MONICA AZARIA MUHOGA | DSM |
| 36 | BALBINA FRANCIS TAIRO | DSM | 75 | DATIVA PETER TEMU | DSM |
| 37 | THERESIA THOBIAS ITAMBIKO | DSM | 76 | MARY SAMWEL NUNGU | DSM |
| 38 | DEVOTA JOSEPH NJAU | DSM | 77 | GLORY JULIUS MBAGA | DSM |
| 39 | INOSENSIA FOT MONDENI | DSM | 78 | LUCY JEREMIAH SENG'UNDA | DSM |
| 40 | TABU YUSUPH JAMBIA | DSM | 79 | PAMELA E SAIMON | DSM |
| | Tujijenge Tanzania Financial Services Ltd, Simu: 0718068335 au **E-mail: tujijengetanzania@tujijenge.or.tz** | DSM | 80 | YAHAYA HASANI MUSA | DSM |

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanawake jitokezeni kuwania nafasi uchaguzi Serikali za Mitaa

**MCHAKATO** wa uchaguzi wa serikali za mitaa unatarajia kufanyika mwezi Novemba mwaka huu na uchaguzi huu uwe chachu ya kuwaibua wanawake wengi kushiriki kuwania nafasi za uongozi.

Wakati wa wanawake kutumika kama wapiga kampeni na kuwa ngazi za kupandisha wenzao kugombea nafasi hizo umepitwa.

Ni haki ya kila mmoja kushiriki kupiga kura na kuchaguliwa, hivyo wanatakiwa kuamka na kujitokeza kwa wingi.

Huu ni wakati wa kuonesha kuwa wanawake wanaweza kupambana na kushinda kwenye chaguzi kutokana na watakavyoweza kujieleza na kumwaga sera zao.

Kukatishwa tamaa kuwe mwiko kwao na wasikubali kuwekewa vikwazo vya aina yoyote ile.

Wengine wanakosa ujasiri wa kuthubutu baada ya kuona wenzao wanavyopata misukosuko ikiwamo kudhalilishwa na kutukanwa kwenye majukwaa.

Hali hiyo inathibitishwa na baadhi ya viongozi wanawake waliowahi kushika nyadhifa za juu serikalini na kwenye taasisi mbalimbali, mikikimikiki waliyopambana nayo mpaka kufanikiwa kushika uongozi.

Miongoni mwa sababu zinazowadhoofisha wanawake wengi kujitokeza kuwania nafasi iwe kwenye siasa au taasisi ni kuombwa rushwa ya ngono.

Kuna wanawake wanaojitambua ambao wakishatajiwa suala la rushwa ya ngono, anaona isiwe tabu na kuamua kuendelea na mambo mengine. Sehemu yoyote linapokuja suala la kupewa nafasi kwa upendeleo, ufanisi hukosekana kwasababu ya kukosekana heshima.

Hii ni vita kubwa na inapaswa kukomeshwa na wanawake wenyewe kwa kujitambua na kutokubali kudhalilishwa kwa namna yoyote ile.

Kwenye nafasi za kisiasa, wanawake wengi hulalamika kufanyiwa vitendo vya udhalilishaji kwa kuitwa majina ya ajabu ajabu ili tu wakatishwe tamaa.

Kwa wanawake walio kwenye ndoa wanakuwa kwenye mtihani mkubwa baada ya wenza wao kusikia yanayofanyika kwenye mchakato wa kuwania nafasi hizo na kuamua kuwakataza ili kuepuka kashfa.

Suala hili linahitaji kukemewa na pia elimu ya kutosha kuanzia mijini na vijijini ili wanawake wengi waelimike na kujitokeza kuwania nafasi.

Vyama vya siasa, wanaharakati wa haki za binadamu mna kazi kubwa ya kutoa elimu kupiga vita jambo hilo.

Kwa kudhoofisha wanawake kujitokeza kuwania nafasi za uongozi, kunaweza kukapoteza ari yao ya kuonyesha vipaji vyao vya uongozi.

Na katika maeneo mengi ya kazi imeshuhudiwa kuwa wanawake wanapopewa uongozi wanafanya vizuri na hata suala la rushwa ya ngono huwezi kulisikia. Mapambano ya rushwa ya ngono ni lazima yawe makubwa ili kukomesha hali hiyo kabisa.

Aidha, wanawake wajitahidi kuhamasishana wajitokeze kugombea nafasi mbalimbali wasibakie kuwa wapigakura.

Katiba inaruhusu kugombea, kupiga kura na kupigiwa, lakini bado hawajitokeza kwa hofu ya udhalilishaji.


"Vikwazo vipo vingi vinavyowafanya wanawake washindwe kujitokeza kugombea, sababu moja wapo hatuna uthubutu, pili, elimu ya uraia haiwafikii kinamama nje ya miji, juhudi zifanyike wafikiwe. Rushwa ya ngono ni kikwazo, waume zetu wakisikia unataka kugombea wanakukataza kama haujaolewa wazazi wanakukataza kugombea," anasema aliyewahi kuwa waziri wa zamani Shamim Khan.

Mwanamke akitaka kugombea nafasi yoyote anapaswa kukataa rushwa ya ngono na akiwa na heshima yake hakuna atakayemfuata.

Pia, ni muhimu wakajua kanuni na vyama vya siasa vifanye bidii kupeleka kanuni hizo hadi ngazi ya chini ndipo watapatikana wanawake wengi.

Kuna nafasi za viti maalum vya udiwani na ubunge, ambazo zimependekezwa na wadau wa siasa ziwe na ukomo wa miaka kumi ili kutoa nafasi kwa wanawake wengine kuziwania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Sungusungu wanaojifanya mahakama, hiyo haikubaliki

Na Adam Fungamwango

**KUMEKUWA** na tabia ya baadhi ya walinzi jadi, maarufu kama sungusungu kwenye mikoa mbalimbali nchini kufanya kazi zisizowahusu, ambazo sizo wanazotakiwa kufanya.

Walinzi hao ambao mijini wanajulikana kama Polisi Jamii, baadhi ya mikoa wamekuwa wakifanya kazi ya kukamata wahalifu lakini hao hao pia wamekuwa wakijifanya mahakama na kutoa adhabu.

Hiki kimekuwa ni kilio kikubwa kwa wananchi wanaokutana na adha hiyo, ambapo pamoja na mambo mengine wamekuwa wakikutana na adhabu kubwa kuliko kosa walilolifanya, kutengwa na jamii na adha zingine zinazofanana na hilo.

Jeshi hilo la Sungusungu limeanzishwa kwa sababu ya kulinda usalama wa raia na mali zao, kusaidia maeneo kuwa na amani na utulivu, kuzuia uhalifu, lakini wanapowakamata au kukuta kuna uhalifu wanatakiwa kuwaona askari polisi, au kuwapeleka kituoni wahalifu.

Matokeo yake, baadhi yao ambao si waaminifu wamegeuza kuwa mradi kwani wanawaadhibu watu kwa kuwapiga faini mifugo kama mbuzi, ng'ombe, mazao, wakitumia bakora, au kuwaambia wanakijiji wamtenge kwenye shughuli za kijamii na yoyote atakayekiuka naye ataadhibiwa.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha, ameliona hili na kulikemea vikali. Alizungumza katika mkutano wa hadhara juzi kwenye kijiji cha Manyanda mkoani Shinyanga, alisema kumekuwa na tabia ya sungusungu kutoa adhabu kwa wananchi ikiwamo kuwatenga kutojihusisha na chochote ndani ya jamii.

Akasema kwa mujibu wa sheria za nchi, jukumu la kutoa hukumu ni la mahakama pekee na si mtu yeyote.

**Akasema kwa mujibu wa sheria za nchi, jukumu la kutoa hukumu ni la mahakama pekee na si mtu yeyote. Alisema serikali inatambua mchango wa jeshi hilo la jadi sungusungu la kuhakikisha amani na utulivu utawale ndani ya jamii na kudhibiti vitendo vya kihalifu, lakini wanapokuwa katika majukumu yao, wahakikishe wanazingatia sheria za nchi.**

Alisema serikali inatambua mchango wa jeshi hilo la jadi sungusungu la kuhakikisha amani na utulivu utawale ndani ya jamii na kudhibiti vitendo vya kihalifu, lakini wanapokuwa katika majukumu yao, wahakikishe wanazingatia sheria za nchi.

Binafsi nampongeza mkuu wa mkoa huyo, na alichokisema hakipo kwenye kijiji hicho au mkoani mwake tu, bali mikoa mingi na vijiji vingi nchini.

Haiwezekani mtu anayekamata ndiyo anayetoa hukumu na adhabu. Ndiyo maana utaona hata askari polisi wakikamata wahalifu wanawapeleka mahakamani, siyo wao wanaowahukumu, ndipo kuna chombo cha kutafsiri hukumu. Na hata mtu akihukumiwa siyo mahakama inayomweka kwenye magereza yake. Mahakama haina magereza, bali kuna Jeshi la Magereza, ambalo nalo liko kivyake. Yenyewe inapewa tu mtu ambaye amehukumiwa.

Hapo utaona kuna taasisi tatu tofauti na hii yote ni kumfanya yeyote awe na haki, na kuzuia visasi, chuki na kukomoana. Waliokaa kutengeneza mfumo huo hawakufanya hivyo kwa bahati mbaya.

Binadamu anatakiwa kuhukumiwa kutokana na uzito wa kosa alilolifanya, sungusungu wanatoa adhabu kubwa kwa kosa dogo tu, pia adhabu siyo kumkomoa mtu, bali ni kumkumbusha kuwa alichokifanya si sahihi, ndiyo maana mahakimu hutoa adhabu kulingana na kosa alilofanya mtuhumiwa na si vinginevyo.

Nadhani kuanzia sasa sungusungu wenye tabia hii wamulikwe na kuchukuliwa hatua ili raia wakae kwa amani na utulivu kwenye nchi yao huru.

HABARI KITAIFA

# Vituo vya kujaza gesi magari kuongezwa

Na Gwamaka Alipipi

IDADI ya vituo vya kujaza gesi katika magari vinatarajiwa kuongezeka kutoka vitatu vya sasa hadi 13 mkoani Dar es Salaam ifikapo Juni mwakani.

Mkakati huo unalenga kumaliza mateso ya madereva wa magari na bajaji kukaa kwenye foleni kwa muda mrefu pindi wanapohitaji kujaza nishati hiyo.

Kaimu Mkurugenzi wa Biashara ya Gesi na Mafuta wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Emmanuel Gilbert alitoa ufafanuzi huo jana jijini Dar es Salaam wakati anazungumza na waandishi wa habari baada ya juzi kutokea foleni ndefu ya kujaza gesi katika vituo maalum vilivyoko jijini.

Alisema foleni iliyotokea katika vituo vya kujaza gesi vya Ubungo na Uwanja wa Ndege ilisababishwa na hitilafu ya umeme katika kituo cha kujaza gesi kilichoko eneo la Tazara jijini.

Ni hitilafu anayoitaja ilitokea usiku wa kuamkia juzi na ilidumu kwa saa 21; imeshatatuliwa na huduma zinaendelea kutolewa.

Alisema hitilafu hiyo ilitokea katika kituo cha Tazara ambacho hakina mfumo mbadala wa kujiendesha pindi kunapotokea tatizo la umeme.

Gilbert alisema Mkoa wa Dar es Salaam una vituo vitatu pekee vya kujazia gesi, hivyo kimojawapo kikipata hitilafu, kunakuwa na msongamano kwa vyombo vya moto katika vituo viwili vilivyobakia kunakosababishwa na kushindwa kuhimili idadi ya wahitaji.

Ofisa huyo wa TPDC alisema: "Lengo la serikali ni kuhakikisha watumiaji wa vyombo vya moto vinavyotumia gesi, wanapata huduma ya uhakika. Hivyo, ifikapo Juni mwakani, tunatarajia kuwa na vituo 13."

Alisema kuwa katika kutatua kero ya uhaba wa vituo vya kujaza gesi, serikali imeshatoa leseni kwa kampuni binafsi 40 ambazo zimeonesha nia ya kujenga vituo hivyo.

Mkurugenzi huyo alisema changamoto inayosababisha sekta binafsi kushindwa kujenga vituo vya kujaza gesi kwa wingi kama ilivyo vituo vya mafuta, ni gharama za ujenzi wa kituo.

Alisema ujenzi wa kituo kimoja cha kujaza gesi unagharimu kati ya Sh. bilioni 2.1 na Sh. bilioni 2.7 kulingana na ukubwa na mahitaji ya eneo wakati kituo cha mafuta ni Sh. milioni 400.

Ofisa huyo alisema kuwa sasa idadi ya magari yanayotumia mfumo wa gesi nchini ni zaidi ya 4,800, lakini uwezo wa vituo vya kujaza gesi ni kuhudumia magari 1,200 hadi 1,500 kwa siku.



Mteja akichagua mbuzi katika mnada wa Vingunguti, jijini Dar es Salaam jana. Bei ya kitoweo hicho, imeonekana kushuka kutoka 120,000/- kwa 150,000/- hadi 80,000/- kwa 100,000/- kwa mbuzi mmoja kulingana na ukubwa wake. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mahakama ya Mafisadi yaamuru nyumba, fedha na gari vitaifishwe

NA Kulwa Mzee

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, maarufu Mahakama ya Mafisadi, imemtia hatiani mfanyabiashara Oje Boniface, raia wa Nigeria na kumuhukumu kifungo cha miaka tisa gerezani na kuamuru nyumba, gari na fedha zitaifishwe na serikali.

Hukumu hiyo ya mahakama ilisomwa juzi mbele ya Jaji Godfrey Isaya baada ya mshtakiwa kupitia Wakili wake Lovenes Ngowi kukiri kosa.

Akisoma hukumu hiyo, Jaji Issaya alisema mshtakiwa aliingia maridhiano na Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP) kukiri kosa la kusafirisha dawa za kulevya aina ya cocaine gramu 420.33.

"Kukiri kosa ni sehemu ya maridhiano, pande zote mbili ziliomba ziongozwe na mkataba wa maridhiano.

"Mahakama inabidi kufuata maridhiano kwa kuwa sehemu ya makubaliano mshtakiwa atumikie kifungo cha miaka 12 badala ya miaka 30 au maisha na kwamba katika kutoa adhabu hiyo miaka mitatu aliyokaa ndani izingatiwe.

"Mahakama inapunguza miaka mitatu, hivyo mshtakiwa atatumikia kifungo cha miaka tisa jela," alisema Jaji Isaya.

Alisema mahakama inatoa amri dawa za kulevya gramu 316.40 na gramu 103.93 ziharibiwe kwa kuchomwa moto.

"Kipande cha ardhi chenye nyumba iliyoko maeneo ya Mbezi Makabe, gari lenye namba ya usajili T 414 DQF Toyota Premium zinataifishwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania," alisema.

Jaji Isaya alisema mshtakiwa anatakiwa kuzingatia vigezo vyote vilivyoko katika mkataba na ana haki ya kukata rufani kwa adhabu peke yake.

Katika kesi hiyo, Jamhuri iliwakilishwa na Wakili wa Serikali Martietha Magata, aliyedai kuwa mshtakiwa alikuwa anakabiliwa na shtaka moja la kujihusisha na biashara haramu ya kusafirisha dawa za kulevya.

Alidai kuwa mshtakiwa alikamatwa Mei 24, 2021 akiwa na dawa za kulevya aina cocaine gramu 316.40 ndani ya gari na alipokwenda kupekuliwa nyumbani kwake Mbezi Makabe, wilayani Ubungo, alikutwa na gramu 103.93.

Mshtakiwa aliposomewa maelezo ya awali, alikiri kukutwa na dawa hizo na kwamba wakati anakamatwa alikuwa na umri wa miaka 32.

Mshtakiwa pia alikiri kukutwa na fedha taslimu Sh. 310,000, fedha za Malawi 7,200, fedha za Kenya Sh. 50 pamoja na dawa za kulevya ambapo vyote kwa pamoja na mkataba wa mauziano ya ardhi na kadi ya gari vilitolewa mahakamani kama vielelezo namba moja na pili.

Mahakama iliamuru dawa zifunguliwe na zilifunguliwa, mshtakiwa na wasikilizaji walishuhudia zikiwa katika muundo wa mipira midogo minne.

Baada ya kutiwa hatiani, upande wa Jamhuri uliomba amri ya kuharibiwa dawa, pia ukaomba nyumba, gari na fedha zitaifishwe kuwa mali ya serikali.

Wakili Marietha alidai Jamhuri inaamini fedha zilitokana na mazalia ya biashara haramu ya dawa za kulevya.

Wakili Lovenes Ngowi, akimtetea mshtakiwa apunguziwe adhabu, alidai ni mkosaji wa mara ya kwanza, familia inamtegemea, ana watoto watatu na mke na kutokana na makubaliano aliyoingia, familia haina nyumba ya kuishi.

Aliomba mahakama impunguzie adhabu, impe kifungo cha muda mfupi ili akae kidogo gerezani arudi kuhudumia familia yake.

Mahakama ilizingatia hoja zote, ilimtia hatiani na kumhukumu kwenda jela miaka tisa na mali zake ambazo ni nyumba, gari na fedha alizokutwa nazo zinataifishwa na serikali.

Dawa alizokutwa nazo zitahifadhiwa kusubiri utekelezaji amri ya kuziharibu kwa kuzichoma moto.

KABWELA Na Fadhili Mohammed





Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Ashatu Kijaji (mwenye hijab), akikagua athari za kimazingira katika Mto Segerea, wilayani Ilala, jijini Dar es Salaam juzi, wakati wa ziara ya kikazi. Wengine ni Naibu Waziri wake, Khamis Hamza Khamis (wa pili kushoto) na watendaji kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC). **PICHA: OMR**

HUKUMU KESI BINTI WA DOVYA

# Wakili: Hakuna ushahidi 'afande' kuunganishwa

**Na Christina Mwakangale**

WAKILI Edwin Mugambila, amesema sababu ya mtuhumiwa anayetajwa kwa jina la 'afande', kutounganishwa katika kesi ya kubaka kwa kundi na kumwingilia kinyume cha maumbile binti mkazi wa Yombo Dovya, Dar es Salaam, kunatokana na ushahidi duni na kukosa muunganiko wa picha na afande.

Amesema licha ya umma hususan kwenye mitandao ya kijamii kupaza sauti kudai mtu anayetajwa kuwa ni afande alihusika kuwatuma vijana hao wanne waliokutwa na hatia mwishoni mwa wiki, ushahidi ulikosa muunganiko kati ya anayetajwa na picha aliyooneshwa binti, ili athibitishe.

Wakili huyo akizungumza jana, kupitia redio ya Clouds Fm, jijini Dar es Salaam, alisema kesi hiyo ilibeba hisia kali kijamii kulikuwa na maombi takribani 20 yaliyowasilishwa mahakamani, huku makundi ya mawakili zaidi ya matatu yakiomba kuifuatilia, huku ikiendeshwa kwa takribani miezi miwili hadi hukumu, akisema, lengo ni kumpunguzia msongo mtendewa.

"Binti (binti wa Yombo) mwenyewe tulipomhoji alisema picha aliyoonyeshwa kwamba ndiye afande alikuwa jinsi ya kiume, mijadala ilikuwa ni mingi na hisia zilikuwa nyingi. Hata sisi (mawakili) ilituletea confusion (mkanganyiko) sana.

Binti, wakati wa tendo likiendelea alikuwa anaambiwa 'muombe msamaha huyu...' mimi sikuiona hiyo picha, ila kinachoelezwa na wahusika wakati wa kuchambua ushahidi, washtakiwa wenyewe Nyundo na wenzake, walisema ilikuwa picha ya mmoja wetu (washtakiwa).

Lakini sasa pamoja na hiyo 'confusion' mnafanyaje, mnahitaji japo chembe ya kum-konekti huyu mtu (afande) na tukio? Ili kupambana huyu mtu aletwe mahakamani kama mshtakiwa. Kulikuwa hamna muunganiko," alisema wakili huyo ambaye ni Mkurugenzi wa Mtandao wa Kitaifa wa Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu.

Kinachoelezwa ni kwamba walichukuana baa (binti na washtakiwa) kwa maandalizi fulani fulani, wameanza kumfanyia kile kitendo wakimwonesha picha, huku wakimtaka aombe msamaha kwa picha ya mwanamume, haijulikani alikuwa ni nani ila ni miongoni mwao.

Sasa ili yule mama (anayetajwa kuwa afande), aingie katika mashtaka ni lazima mmoja wa wale vijana wamtaje au shahidi yeyote, tofauti na hapo atatajwa yeyote kama hakuna ushahidi, hakuna muunganiko wa tukio hata sisi wenyewe tulitaka apelekwe mahakamani, lakini ushahidi uko wapi, labda kitakachofanyika ni ushahidi wa kimazingira."

Alisema kuhusu adhabu zilizotolewa dhidi ya washtakiwa hao, mbali na kifungo cha maisha jela, Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai Kifungu cha 348, kinatoa mwongozo kwa makosa ya kijinsia 'sexual offences' ni lazima mwathirika kupewa fidia.

"Kiasi gani cha fidia anatakiwa apewe, hilo ni kwa jaji au hakimu, ndio maana akatoa amri wale vijana wote watoe shilingi milioni moja kila mmoja. Ingawa kuna madhara amepata huyo binti, madhara iliyopata familia wanaweza kufungua shauri la madai, kwa madhila aliyopitia, msongo na muda aliopoteza na mahangaiko kifamilia," alisema wakili huyo. "Inategemeana na wanaweza kuomba fidia ya kiwango chochote hata Sh. bilioni 200 kutokana na tathmini ya mahakama ya madhara aliyoyapata, itakavyoona inafaa. Na kama wana mali waliohukumiwa...au kwa nchi zilizoendelea kuna mfuko maalum wa fidia kwa waathirika wa matukio kama hayo.

Au njia ya pili kama waliohukumiwa wana mali, zile mali zinakamatwa na kuuzwa kulipia fidia. Kwa uzoefu tulionao ni nadra hili kutokea, ila kwa kuwa anasimamiwa na taasisi za kisheria, tuna imani wanaweza kusimamia hilo."

Washtakiwa wanne katika kesi ya kubaka kwa kundi na kumwingilia kinyume cha maumbile binti mkazi wa Yombo Dovya, Dar es Salaam, mbele ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma, wamehukumiwa kifungo cha maisha jela, hivi karibuni.

Washtakiwa hao walikuwa ni Askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), MT 140105 Clinton Damas, maarufu Nyundo na Amin Lema, maarufu Kindamba.

Wengine ni Askari Magereza C.1693 Praygod Mushi pamoja na Nickson Jackson, maarufu Machuche.

Agosti 19, mwaka huu, washtakiwa hao walifikishwa katika mahakama hiyo wakikabiliwa na mashtaka mawili ya kubaka kwa kundi na kumwingilia kunyume cha maumbile binti huyo.

Kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16, iwapo wakithibitika kutenda ukatili huo, watakumbana na adhabu ya kifungo cha maisha gerezani.

# TFS yaweka kambi kudhibiti uchomaji moto holela misitu

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) imeweka kambi ya wiki maalumu kwa ajili ya kampeni ya mapambano ya kudhibiti vitendo vya uchomaji moto holela vinavyofanywa na baadhi ya wananchi kwenye milima ya Uluguru na maeneo mengine ya Mkoa wa Morogoro.

Kampeni hiyo iliyopewa jina la "Usianzishe moto usiouweza kuuzima kuwa mwenye tahadhari ya moto" inashirikisha wananchi wa kata ya Mlimani na Boma zilizoko Manispaa ya Morogoro ambazo zipo ndani ya mlima huo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti kwa niaba ya wananchi, wenyeviti wa mitaa ya Kibwe na Mbete iliyopo kwenye kata hizo walisema kwenye mitaa yao wameunda kamati za mazingira zinazowashirikisha vijana zenye jukumu la udhibiti wa moto na ufuatiliaji kwa wanaoandaa mashamba kwa kutumia kuchoma moto majani.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Kibwe, Kata ya Boma, Thobias Augostino, alisema wameamua kuweka ushirikiano na wenzao wa mitaa ya kata ya Mlimani ili kuzuia viashiria vyoyote vya watu wanaotumia moto pasipo kutoa taarifa katika kamati zao ili tahadhari ziweze kuchukuliwa.

"Zipo sheria ndogo za mazingira ikiwamo ya kuwasha moto ovyo endapo mtu akivunja sheria anaadhibiwa kulingana na makosa yaliyotendeka," alisema Thobias.

Naye Mwenyekiti wa Mtaa wa Mbete, Kata ya Mlimani, Feruzi Mohamed, alisema wapo kwenye mkakati wa kutunza na kuhifadhi mazingira na kwa miaka mingi hakuna matukio ya uanzishwaji wa moto.

Alisema kamati za mazingira zipo makini kudhibiti moto na ufuatiliaji wananchi wanapoandaa mashamba na zinachukua jukumu la kuwashauri wananchi kuchukua tahadhari ya moto usilete madhara katika misitu ya asili na hifadhi.

Hata hivyo, alisema wataendelea kuwa walinzi wazuri katika kuthibiti vitendo vya uchomaji moto kwenye misitu ya asili na ya hifadhi ya milima Uluguru ambayo ni tegemeo kubwa kijamii na kiuchumi.

Naye Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule ya Msingi Mbete, Jonson Mremi, alisema kuwa wamekuwa na vipindi vya elimu ya mazingira kwa wanafunzi wa shule hiyo ili kuwarithisha rasilimali za maliasili kwa ajili ya manufaa yao ya baadaye.

Alisema licha ya vipindi vya elimu ya mazingira, shule hiyo ina kitalu cha miche ya miti kwa ajili ya kupanda kuzungumza eneo la shule na majirani ikiwa na kuwaelekeza wanafunzi kutambua elimu ya mazingira na kupiga vita vitendo vya uharibifu na uchomaji moto misitu.

Mhifadhi wa TFS, Shaaban Kiula kutoka Kanda ya Mashariki, aliwakumbusha wananchi wa kata hizo na nyingine kutambua jukumu la utunzaji wa mazingira na misitu si la serikali pekee bali pia ni la jamii.

Kiula alisema ni vyema kila mwananchi awe na uchungu wa kulinda na kuisimamia rasilimali ya misitu, kutii sheria bila shuruti na kuchukia pale moto unapojitokeza ndani misitu ya asili na ya uhifadhi.

"Iwapo uharibifu huo unaotokana na uchomaji moto unachangia kuleta madhara makubwa kwa viumbe hai wengine na kusababisha ukosefu wa mvua zisizotabirika na vyanzo vya maji kukauka," alisema Kiula.

Chanzo cha moto kwenye milima ya Uluguru kinachangiwa na baadhi ya wananchi kufanya shughuli za kibinadamu zikiwamo za kuandaa mashamba kwa kutumia moto na uchomaji mkaa na wanaoshindwa kuudhibiti unakwenda kuunguza misitu ya asili na hifadhi ya milima hiyo.

# Babu apigia debe kilimo hai

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, ametaka suala la usalama wa chakula litazamwe kwa jicho la tatu na wakulima wadogo, kuanzia uzalishaji, uchakataji na usindikaji wa mazao ya mboga, viungo na matunda ili kulinda afya za walaji dhidi ya magonjwa ya saratani, moyo na ngozi.

Akizungumza jana mjini hapa na vikundi vya wakulima wakati wa maonyesho ya mbegu yaliyoandaliwa na Shirika la Floresta Tanzania kwa kushirikina na Shirika la World Vegetable Center kupitia Mradi wa Kupeleka Teknolojia Haraka kwa Wakulima (AID-I).

Babu alisema kuwa ametoa kauli hiyo kutokana na idadi kubwa ya watu kula vyakula ambavyo vina kemikali nyingi, kuliko ambavyo vilikuwa vikizalishwa zamani kwa njia ya kilimo hai.

Alisema suala hilo la usalama wa chakula ni ajenda ya kimataifa na Tanzania inaunga mkono.

AID-I ni sehemu ya mpango wa kimataifa chini ya msaada wa Serikali ya Marekani (USAID) wa kukabiliana na njaa na umaskini, ukilenga kutoa msaada kwa wakulima wadogo katika nchi za Tanzania, Malawi na Zambia na kuhakikisha wanapata teknolojia, ubunifu na taarifa zinazohitajika haraka ili kuongeza na kuimarisha uzalishaji wa chakula," alisema Babu na kuongeza kuwa:

**"Floresta Tanzania na World Vegetable Center, kupitia mradi huu wa AID-I wameamua kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa mbegu bora, mnyororo wa thamani wa mboga na viungo ka-**

"Floresta Tanzania na World Vegetable Center, kupitia mradi huu wa AID-I wameamua kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa mbegu bora, mnyororo wa thamani wa mboga na viungo katika Mkoa wa Kilimanjaro. Juhudi hizi zinalenga kuongeza uzalishaji wa mboga kwa lengo la kuboresha lishe na kuongeza kipato, ajira kwa vijana, akina mama na jamii ya watu wenye ulemavu.

"Niwapongeze kwa kuunda vikundi vya uzalishaji wa mboga na matunda, mnahamasisha uzalishaji na upatikanaji wa mbegu bora na kuimarisha lishe ya familia. Suala la lishe Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan imeliwekea mkazo mkubwa ili kukabiliana na udumavu na utapiamlo," alisema.

Mkurugenzi wa Floresta Tanzania, Richard Mhina, alisema AID-I unalenga kuwafikia watu 5000 kutoka Kilimanjaro, kati ya hao, asilimia 60 ni vijana na 40 watu wenye umri mkubwa.

Alisema mradi huo pia unalenga kuwawezesha vijana na wanawake kuwa wahamasishaji wakuu wa sekta ya kilimo na maendeleo ya jamii.

"Mradi huu pia unasaidia kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi na kupanda kwa bei za vyakula, mafuta na mbolea kutokana na changamoto za kimataifa kama uvamizi wa Urusi na Ukraine," alisema Mhina.

Maonyesho hayo yalitanguliwa na kauli mbiu 'mbegu zetu, maisha yetu, panda leo kwa kesho endelevu'.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akiwa na Spika wa Bunge ambaye ni Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Dk. Tulia Ackson (kushoto), pamoja na viongozi mbalimbali, baada ya kuwasili kwa ajili ya kufungua Mkutano wa 53 wa Mwaka wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola Kanda ya Afrika, jijini Arusha jana. **PICHA: OMR**

## Wasimamizi uchaguzi mitaa wafundwa

**Na Steven William,** MUHEZA

MSIMAMIZI wa Uchaguzi Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Dk. Jumaa Mhina, amewataka wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi wa serikali za mitaa kuzingatia maelekezo ili kudumisha amani na utulivu wilayani hapa.

Rai hiyo aliitoa mapame wiki hii wakati akifungua semina ya wasimamizi hao iliyofanyika mjini hapa.

"Kila mtu anajua kwanini ameteuliwa na mmeaminiwa kula kiapo kuwa mtalivusha salama taifa katika zoezi linalokuja mbele yenu na mjue kwa sasa macho na masikio ya watu wote yapo kwenu msituangushe," alisema Dk. Mhina.

Alisema uchaguzi huo upo kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo, hivyo wanapaswa kuzingatia, vinginevyo watawajibika.

Alisema wasimamizi hao wanatakiwa kuwa makini kwa kutekeleza majukumu yao kwa weledi na uzalendo.

Mhina, alisema Muheza ina vijiji 126, 2024 vitongoji 494 na kata 37 ambazo zitashiriki uchaguzi huo wa serikali za mitaa mwaka huu utakaofanyika nchini mwezi ujao.

Kwa upande wake, Ofisa Uchaguzi wa wilaya hiyo, Zaituni Abdul Said, aliwahimiza wasimamizi hao kuwahi kufungua vituo vyao vya kazi siku ya kuanza uandikishaji.

# EU yapiga jeki mfumo wa malipo EAC

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

UMOJA wa Ulaya (EU) umetoa dola milioni 25 za Marekani kwa ajili ya kusaidia uundaji mfumo salama wa kidijitali, hasa biashara kwenye mfumo wa malipo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Hayo yalisemwa jana jijini hapa na Naibu Katibu Mkuu wa EAC, Annette Ssemuwemba, wakati wa mkutano wa EU na jumuiya hiyo kujadili uudwaji wa mfumo huo.

"Hivi sasa ni enzi ya kidijitali, na kama EAC ni lazima tuweze kuendelea. Tuko katika harakati za kukamilisha mkakati wetu wa mabadiliko ya kidijitali, na hii imeundwa kuzunguka nguzo nne.

"Nguzo moja ni E commerce, na unajua ni biashara na biashara zetu zinahitaji kufanya biashara kidijitali. Nguzo ya pili ni kwenye mifumo ya malipo," alisema Ssemuwemba.

Alisema ni muhimu kufanya malipo kidijitali kwa kutumia simu zetu, kielektroniki, kwa kutumia kompyuta zetu, bila kulazimika kwenda benki.

Alisema ili kufikia hatua hizo ni lazima nguzo hizo zilindwe kwa kuhakikisha usalama wa mtandao upo vizuri na kila anayefanya miamala hiyo inakuwa salama.

"Na nguzo ya mwisho ya serikali ni sisi sote, kama serikali tunafanya kazi pamoja ili kuhakikisha kuwa raia wetu ni raia wa kidijitali," alisema.

Alisema mkutano huo umeshirikisha nchi wanachama wa EAC na nchi washirika zinawakilishwa na umoja huo kutoka Ufaransa, Ujerumani, Estonia na nyingine wanachama wake wa EAC, wakiwamo wajumbe kutoka EU wenye makao makuu jijini Dar es Salaam.

Alisema nchi hizo zimeshiriki ili kupitia kila nguzo na kutengeneza kile kinachohitajika kutelekezwa mara moja.

Msimamizi wa Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) EAC, Daniel Murenzi, aliushukuru EU kwa kutoa fedha hizo kuunganisha mfumo huo na kuwa mmoja katika nchi hizo ili kupunguza usumbufu kwa wananchi wanaposafiri.








Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT), Dk. Florian Mtey (kushoto) na Mkurugenzi wa Mahusiano wa SBL, John Wanyancha (kulia), wakitiliana saini hati za makubaliano ya ushirikiano, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii, kwa ajili ya kuwapa wanafunzi na wahitimu wa fani ya ukarimu ujuzi muhimu na uzoefu wa vitendo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Aua mke, ajimaliza kwa pombe, vidonge

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MFANYABIASHARA Devrinus Nkabatina (46), Mkazi wa Nyamhongolo Wilaya ya Ilemela mkoani hapa, anadaiwa kumuua mkewe, Rausa Mohamed (36) kutokana na wivu wa mapenzi kisha kujiua kwa vidonge na pombe kali.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Wilibroad Mutafungwa, alisema juzi kuwa walipokea taarifa za mtuhumiwa huyo kumuua mkewe Septemba, 28 majira ya saa 4:45 usiku kutoka kwa majirani zao.

Mutafungwa, alisema inadaiwa kuwa kabla ya mauaji hayo, kulikuwa na ugomvi baina ya wanandoa hao kutokana na mke huyo kumtuhumu muwewe alikuwa na uhusiano wa mapenzi na wanawake wengine.

Alisema baada ya kuibuka mzozo baina ya wanandoa hao, mume huyo alimsukuma mkewe na kumwangusha sakafuni kisha kumchoma na kisu chenye ncha kali kisogoni.

**Alisema baada ya kuibuka mzozo baina ya wanandoa hao, mume huyo alimsukuma mkewe na kumwangusha sakafuni kisha kumchoma na kisu chenye ncha kali kisogoni.**

Mutafungwa, alisema baada ya majirani kusikia mzozo huo, walifika nyumbani kwa wanandoa hao na kumkuta mkewe huyo akiwa amejeruhiwa vibaya, na kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi.

Alisema majirani hao walimchukua mke huyo na kumpeleka Kituo cha Afya Igoma na kufa wakati madaktari wakimpatia matibabu.

Alisema mtuhumiwa huyo alitoweka baada ya tukio hilo na kutokomea kusikojulikana.

Alisema jitihada za polisi kumtafuta mtuhumiwa huyo zilianza baada ya kupata taarifa za kutokea kwa kifo hicho.

Alisema wakati wakiendelea na msako dhidi yake, Septemba, 30, mwaka huu, majira ya mchana, walipata taarifa kuwa mtuhumiwa huyo yuko baa anakunywa pombe.

"Polisi walifika katika baa hiyo na kumkuta mtuhumiwa amedhoofika," alisema na kuongeza kuwa: "Tulipata taarifa kutoka kwa wahudumu wa baa, Nkabatina alifika ameshika bahasha yenye rangi ya kaki na kuagiza pombe aina ya konyagi chupa kubwa, kisha alimeza vidonge ambavyo idadi yake haikufahamika kwa kutumia pombe aliyokuwa ameagiza ndipo hali yake ilianza kubadilika ikawalazimu watoe taarifa kwa Jeshi la Polisi," alisema Mutafungwa.

Alisema baada ya polisi kumfanyia upekuzi, walimkuta na dawa aina ya Metronidazole na konyagi kwenye chupa.

Kamanda huyo, alisema vilevile walimkuta na karatasi yenye ujumbe usemao 'Shetani ameanza kuniita ewe Mwenyezi Mungu roho yangu naikabidhi mikononi mwako'.

Alisema karatasi hiyo pia ilikuwa na maandishi mengine yaliyosomeka majuto ya kitendo cha kumuua mke wake, amefanya maamuzi ya kujiua na angependa mwili wake usipelekwe kwao Karagwe mkoani Kagera bali uzikwe Mwanza.

Alisema Nkabatina alikimbizwa Hospitali ya Mkoa wa Mwanza Sekeo-Toure kwa matibabu na kufa wakati madaktari wakiendelea kumpatia matibabu.

Alisema uchunguzi wa awali wa polisi umebaini mtuhumiwa huyo alijiua kukwepa mkono wa sheria kwa kumuua mkewe.

## DED ataka weledi mikopo asilimia 10

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Alexius Kagunze, ametaka umakini na weledi katika usajili wa vikundi vinavyotarajiwa kunufaika na mikopo ya asilimia 10 ili kudhibiti udanganyifu kwa kutoa kwa watu wasio sahihi.

Kagunze alitoa kauli hiyo juzi wakati akifungua mafunzo ya kamati za huduma za mikopo ngazi ya kata ya halmashauri hiyo yaliyojumuisha watendaji wa kata, maofisa elimu, kilimo na askari wa Jeshi la Polisi.

Alisema serikali ilisitisha utoaji wa mikopo hiyo kwa vikundi hivyo vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu baada ya kubaini ilikuwa ikitolewa kwa watu wasio sahihi.

Alisema ili kundokana na changamoto, wanatakiwa kusajili vikundi vyenye sifa.

"Lengo la serikali kutoa mikopo hii ni kusaidia makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kujikwamua kiuchumi na kupambana na umaskini," alisema.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii wa Manispaa hiyo, Peres Kamugisha, alisema waombaji wa mikopo hiyo lazima wawe raia wa Tanzania wenye umri wa kuanzia miaka 18.

Kamugisha, alisema vikundi vyao vinapaswa kuanzia watu watano kwa makundi ya wanawake na vijana na watu wenye ulemavu wawili.

# Mpina aibukia kanisani, ataka waumini kugombea mitaa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MBUNGE wa Kisesa (CCM) mkoani Simiyu, Luhaga Mpina, amewataka waumini wa Kanisa la Waadventist Wasabato (SDA), lililoko Kata ya Kagongwa Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga kugombea uongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa nchini Novemba 27, mwaka huu.

Mpina alitoa rai hiyo juzi wakati wa uzinduzi wa albamu ya tatu ya kwaya ya kanisa hilo na harambee ya kuchangia fedha.

Alisema hatua inayoendelea kwa sasa ni maboresho ya daftari la kudumu la wapigakura na la mkazi kwa wananchi kujiandikisha katika maeneo ya kata ili waweze kuchagua wenyeviti wa mitaa, vijiji na vitongoji mwezi ujao.

Aliwataka wananchi kutekeleza wajibu wao kwa kujitokeza kuboresha taarifa zao ili kupata nafasi ya kushiriki chaguzi hizo na kupata viongozi bora watakao waletea maendeleo.

Alisema, uchaguzi wa serikali za mitaa ndio utakaotoa taswila ya uchaguzi mkuu, hivyo kila muumini ana wajibu wa kushiriki kuchagua viongozi wenye sifa, kufanya kazi kwa kujitoa, wenye hofu ya Mungu na sio kutanguliza mbele maslahi.

Mpina, alisema hatua hiyo itasaidia kupambana na migogoro ya ardhi kabla ya kuwafikia viongozi wa wilaya na mkoa.

Alisema waumini wa madhehebu mbalimbali ya dini nchini, nao wanatakiwa kugombea uongozi wa serikali za vijiji, mitaa na vitongoji.

Alisema lengo ni kupata viongozi watakaokuwa wanawasemea inatokea shida kwenye mitaa na kufanya maamuzi yenye hekima kuliko kuacha wanasiasa kuchangamkia fursa hiyo.

Mchungaji wa Kanisa hilo, Mhubiri Ndhobo, alisema kila Jumamosi ya ibada na mafunzo mbalimbali kanisani, amekuwa akiwahamasisha waumini wake kujitokeza kuboresha daftari la kudumu la mpigakura na kushiriki kinyang'anyiro cha uongozi mwezi ujao.

Ndhobo, alisema waumini wake wamekuwa wakimwahidi kuwa watashiriki uchaguzi.

Aliwataka viongozi wa madhehebu mengine kuendelea kuhamasisha waumini wao kushiriki katika uchaguzi huo ili kupata viongozi wanaowataka na sio kuletewa viongozi kwa kuwa maeneo yao yatakosa maendeleo.

Ofisa Uchaguzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Elikana Shija, alisema uboresha wa daftari la kudumu la mpigakura kwa mkoani humo ulifanyika vema na wananchi wengi kujitokeza.



Ukurasa 12

**Wakulima waja na yao, wanataka wapatiwe mbunge wao**




Ukurasa 13

Viongozi wasitumie Polisi kukabili wanaoongozwa


# BUFE

IJUMAA OKTOBA 4, 2024

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




Ukurasa 14

**UZALISHAJI WILAYANI UKIDIDIMIA...**

**Mkuranga washtuka hujuma za korosho kukithiri kila kona zake**

FEDHA

RUSHWA ILIVYO NCHINI...

# Marufuku ya Samia 2021, nchi kung'aa kimataifa na ukakasi wake katika kodi

**Na Neema Emmanuel,** aliyekuwa DODOMA

RUSHWA imekuwa kikwazo katika mfumo wa haki ya kodi nchini, hata kuchangia watoa huduma, viongozi na wafanyabiashara wengi kuamua yasiyo sahihi, ili kupata faida binafsi hali inayoharibu maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Mwaka 2022/23 ya Utendaji Kazi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imetaja udhaifu wa kiutendaji na vitendo vya rushwa katika taasisi za serikali, baadhi ya vigogo wakifikishwa mahakamani na hata kuhukumiwa kifungo gerezani.

Miongoni mwa yaliyobainishwa ni malipo ya fedha za utekelezaji miradi ilhali miradi yenyewe haijatekelezwa, ujenzi holela wa vituo vya mafuta na nyaraka feki kuthibitisha malipo ya safari za nje.

Hilo lipo katika mifumo mbalimbali, kwani hata alipokuwa akikabidhi Ripoti ya Rushwa kwa Rais Samia Suluhu Hassan, jijini Dodoma Machi 28, mwaka huu, aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Kamishna Salum Hamduni, akaitaja miradi iliyofuatiliwa ni pamoja na maendeleo inayotekelezwa kwa utaratibu wa 'Force Account'.

Pia, akataja miradi 12 ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji yenye thamani ya Sh. bilioni 107.4 katika mikoa ya Morogoro, Dodoma, Iringa, Tabora na Mbeya.



Mtaalamu wa Uchumi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Prof. Abel Kinyondo, akitoa elimu katika mafunzo maaluma ya 'uhamasishaji wa rasilimali za ndani'. **PICHA: NEEMA EMANUEL**

Anasema, matokeo ya ufuatiliaji yalionyesha kuwapo mianya ya rushwa, baadhi ya miradi ikionekana kutosajiliwa na Bodi ya Usajili ya Makandarasi na Wakala wa Usalama Mahali Pa Kazi, sambamba na ucheleweshaji malipo kwa makandarasi.

"Matokeo mengine ni malipo kufanyika pasipo kufanyika baadhi ya kazi, malighafi za ujenzi kutopimwa ubora wake kinyume cha mkataba na kutozingatiwa kwa sheria na kanuni za ununuzi wa umma na kuwapo kwa nyongeza ya kazi pasipo kufuata utaratibu," anasema.

Aidha, kunatajwa rushwa sio tu tatizo la kimaadili, pia ni tatizo la kiuchumi na kijamii, rushwa akiitaja inachangia kupunguza mapato ya serikali, miradi kutokamilika na kuwa chanzo cha watoa huduma kushindwa kulipa kodi stahiki kutokana na hongo wanazotoa.

Hiyo ikatajwa kuchangia serikali kukosa fedha ambazo zingetumika katika maendeleo ya jamii, hata kuathiri huduma za kijamii kama vile elimu, afya na miundombinu, ikisababisha madhara makubwa kwa wananchi.

Tatizo hilo linatajwa kuhatarisha kuchangia kuvuruga imani ya wananchi katika mifumo ya kisheria na utawala, pia kutokulipa kodi na kujihusisha na udanganyifu wakikufuata nyanyo za viongozi wao, hali inayozorotesha ukuaji uchumi na inakwamisha juhudi za serikali kuboresha mazingira ya biashara.

Alipohutubia Bunge Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akaeleza dhamira ya serikali kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa kwa kutowaonea aibu viongozi na watumishi wazembe, wezi na wabadhirifu wa mali za umma.

"Tutaendeleza pia juhudi za kupambana na rushwa kwenye utumishi wa umma," akasisitiza Rais Dk. Samia.

Kwa mujibu wa Jarida la TAKUKURU la mwaka huu, inarejea utafiti uliofanywa na Transparency International ya Mwaka 2023 Kwa jina la 'Corruption Perception Index (CPI)' inaonyesha

Tanzania imefanya vizuri na kupata alama 40 na kushika nafasi ya 87 kati ya nchi 180 zilizofanyiwa utafiti, ikilinganishwa na alama 38 ilizopata mwaka 2022 ambapo ilishika nafasi ya 94.

Tanzania, kwa mujibu wa taarifa hiyo, imeshika nafasi ya pili katika mapambano dhidi ya rushwa katika ukanda wa Afrika Mashariki ikitanguliwa na nchi ya Rwanda.


**INAENDELEA UK.14**

UCHUMI

# Wakulima waja na yao, wanataka wapatiwe mbunge wa kuwatetea

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAKULIMA wadogo kutoka Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA), sasa wanaazimia kuitaka serikali iwawekee utaratibu wa kupata nafasi ya uwakilishi bungeni, ili wawe na mtu wa kuwasemea changamoto zao, wakidai ni kutokana na wawakilishi wanaowachagua kutotumia nafasi hizo kwa namna wanavyotaka.

Ni kauli yao wakulima kwenye kongamano la kitaifa la wakulima wadogo linaloenda sambamba na Mkutano Mkuu wa 29 wa MVIWATA, ambao Halima Helela, mmoja wa wakulima anasema ni vema serikali ikaweka utaratibu wa nafasi ya wakulima wadogo bungeni, ili nao wapate wa kuwasemea.

"Ni kweli kuna uwakilishi wa wizara akiwamo Waziri wa Kilimo na wabunge kutoka kwenye kata zetu lakini hatuoni msaada wowote sababu bado tunakabiliwa na changamoto nyingi.

"Tutaendelea kuitwa hatukopesheki hadi lini, benki zilizoko zinakopesha wakulima wakubwa na watu kutoka sekta zingine licha ya kuitwa ni benki ya wakulima..." analalamika Halima.

Mkulima mwingine kutoka mkoani Kagera, Paulina Iseje, anasema wamekuwa wakikandamizwa katika mambo mbalimbali, yakiwamo kisera na sheria ya mbegu imekuwa inawakandamiza, kwa sababu bei ya mbegu imekuwa juu huku mbegu za kuzalishwa na mawakala wadogo (QDS) zikizuiliwa kuvushwa kutoka wilaya moja kwenda nyingine.

"Mbegu za mahindi madukani huuzwa hadi shilingi 20,000 kwa mfuko wa kilogramu mbili huku mkulima akitengeneza kwa kufuata kanuni na taratibu zinazotakiwa na Taasisi ya kuthibiti Ubora wa Mbegu nchini (TOSCI).

"Anaweza kuuza hadi shilingi 4,000 kwa mfuko kwa kilogramu mbili na Watanzania tumezoea kupeana, tunanyimwa uhuru wa kusaidiana, tushirikishwe katika sheria za mbegu," anasema.

Anasema, wakala wakubwa na wenye maduka makubwa ya uuzaji pembejeo za kilimo na mbegu, ni wataalamu wa mbegu na kwamba hali hiyo inasababisha mbegu kuuzwa bei ya juu siku hadi siku jambo linalowakosesha nafasi wao kama wakulima wadogo wenye uchumi wa chini kupata nafuu ya bei ya mbegu.



Baadhi ya washiriki zaidi ya 900 wa Kongamano la Wakulima Wadogo na Mkutano Mkuu wa Mtandao wa Wakulima Wadogo Tanzania (MVIWATA), wakifuatilia mada.

> **"Anaweza kuuza hadi shilingi 4,000 kwa mfuko kwa kilogramu mbili na Watanzania tumezoea kupeana, tunanyimwa uhuru wa kusaidiana, tushirikishwe katika sheria za mbegu.**




Mkurugenzi wa MVIWATA, Steven Ruvuga akiteta jambo na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Alexander Mnyeti, baada ya kufungua kongamano la wakulima wadogo. **PICHA ZOTE: CHRISTINA HAULE**

### WADAU MVIWATA

Awali, Mwenyekiti wa MVIWATA, Apollo Chamwela amesema ipo haja kwa MVIWATA kuona umuhimu wa kutimiza malengo yake waliyoazimia tangu mwaka 2023 ya kuanzisha benki yao ya wakulima ili waweze kupata pa kukopea na kuanza kukua kiuchumi.

Chamwela anasema, mchakato wa kuanzisha benki hiyo upo katika hatua za mwanzo, ambao wana imani utakuwa chachu ya kukua uchumi wa kilimo nchini na kuinua asilimia 75 ya Watanzania waliojikita kwenye shughuli za kilimo kwa manufaa ya taifa.

Mwanachama wa Heshima wa MVIWATA, Bashiru Ally Kakurwa, anawapongeza wakulima kwa kuwa na maono yaliyo wazi, wakitaka mwakilishi bungeni wanayedhani anaweza kuwasaidia kuchambua changamoto zao kisera.

Kakurwa, ambaye ni mbunge wa kuteuliwa na alishakuwa Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), anasema suala la kuhitaji mwakilishi bungeni halihitaji marekebisho ya katiba kwa sasa, bali ifikie mahali vyama vinavyotafuta ridhaa ya wananchi kuingia bungeni, vijitafakari kuwa ajenda zinazobeba kwa uzito maslahi ya wakulima.

Anafafanua kuna aina za wabunge akiwataja; wa kuchaguliwa, kuteuliwa na viti maalum, toa mfanio wa baadhi ya vyama wamewagawa katika makundi yakiwamo viti maalum kwa wenye ulemavu, wafanyakazi, wa vyuo vikuu, wanaotoka mikoani kila mkoa kuwakilisha wanawake mikoani, na vijana.

Kakurwa anasema, jambo hilo sio la kikatiba wala kisheria, hivyo wakati katiba inaangaliwa upya, wanaweza kuangalia suala hilo na kama wanaona linafaa, wasimamishe mwakilishi wa wakulima wadogo bungeni.

"Kwa CCM upande wa wenye ulemavu viti maalum, naona inafanya kazi kubwa bungeni, yupo Keisha yule msanii, Hadija, haaaa likipita jambo pale hata kwa lugha tu ambayo sio sawa kwa wenye ulemavu atasimama kuomba mwongozo wa spika.

"Likija suala la kibajeti au ya ajira, utamwona amesimama na unajua kabisa hapa ni engo ya watu wenye ulemavu, hata wafanyakazi yupo mbunge wa wafanyakazi toka CCM na vijana machachari pia wanaokuja na hoja kubwa, na makundi hayo yakiwakilishwa kuna thamani inaongezeka," anasema.

Hata hivyo, Kakurwa anasema hilo halitoshi kwa sababu uwakilishi haupo bungeni peke yake bali ujumbe huo unapaswa kuwafikia hata viongozi ngazi ya madiwani na Baraza la Wawakilishi Zanzibar na uwakilishi katika ngazi zote hadi vitongoji kwenye serikali za mitaa na vijiji, kuwa wakulima wanataka kusikilizwa na kutatuliwa changamoto zinazowakumba.

Changamoto za wakulima sio kwamba hazitatuliki na hata kama hazitatuliki basi zizungumzike na kujadiliwa, kwa sababu ni hatua ya maana kuelekea kwenye kutafuta ufumbuzi na kuleta maridhiano.

"Pale msimamo wa kiserikali wa kisera au kimaamuzi na msimamo wa wakulima wa uzoefu wao na maarifa yao vikipishana tusione kama jambo la kawaida, kwa sababu tukianza kuzoea kupishana katika mtazamo kijamii tutatengeza hali ya kutoaminiana," anasema.

"Na uongozi wowote usipoaminika, hauwezi kupata uhalali na pale ambapo hakuna uhalali wa kiuongozi wa watu kuridhia jamii hiyo haitawaliki," anaendelea.

Mkurugenzi wa MVIWATA, Steven Ruvuga, anasema kila kauli iheshimiwe na nguvu ya wengi ni kubwa zaidi, kuliko mtu mmoja.

Anasema kuna mitazamo ya kichama kwa ujumla inayomtaka mbunge asimamie na isiwe maslahi ya kundi lake na bora kusimama katika nguvu ya wengi, itakayosaidia kundi lote kusikilizwa kwa pamoja.

Ruvuga anasema, benki nyingi nchini zimechukua mifumo ya benki za nje na kuleta nchini, mara nyingi haziwezi kufanya kazi, kutokana na hali duni za wakulima nchini.

Anasema, anatokana na kuwapo changamoto ya kuwahudumia wakulima kupitia mifumo ya benki, ambayo wamekuwa wakikopesha watu wengine badala ya wakulima.

Kwa mujibu wa Ruvuga, katika kukabiliana na changamoto ya kuwahudumia wakulima kupitia mifumo ya kibenki MVIWATA, imefanikiwa kufanya kazi na Shirika linaitwa ADA na kufanya wakulima kupata mikopo ya shilingi milioni 200 hadi 300 kupitia vikundi vyao mbalimbali.

Hivyo, anaishauri serikali kuangalia jinsi ya kutengeneza mifuko rafiki kwa kundi maalum la wakulima wadogo ili kukabiliana na changamoto zinazojitokeza.

"Hata Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, aliona kuna changamoto ya mikopo ya asilimia 10 kwenye halmashauri ambapo fedha haziendi zinakotakiwa kwa walengwa, nasi kama tukitengeneza mifuko ikawa haiendi kunakohusika itakuwa ni yale yale.

"Kama kutakuwa na mifuko itakayolenga na kuwafikia walengwa itasaidia sana kuongeza kila kinachotakiwa katika uzalishaji ikiwamo tija na uendelevu na ustahimilivu wa wakulima kwa kufidia pale bei za pembejeo zinavyopanda na kushuka," anasema.

Anafafanua kuwa, MVIWATA ina mikakati mbalimbali ikiwamo iliyoanzishwa tangu taasisi ianze mwaka 1993 ambayo ni kutambuliwa kama walivyo na kuheshimiwa, kiutu na hadhi yao.

Ruvuga anasema, wakulima walikabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo kutoheshimiwa na kuonekana kuwa ni watu wasio na uwezo wa kufikiri wala kuamua wenyewe jambo ambalo sio kweli.

Anasema suala la kuangalia mfumo mzima wa chakula na uzalishaji uliojikita katika mfumo tegemezi unaopaswa kugeuzwa na kuwa mfumo wa kujitosheleza kwa ndani kwa kutumia kilimo ikolojia kwa kupokea na kuendeleza dhana ya uhuru wa chakula kwa kutumia rasilimali kuzalisha ambacho kitatumika ndani ya familia yake na taifa kwa ujumla.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Viongozi wasitumie Polisi kukabili wanaoongozwa






NA JOSEPH KULANGWA
(+255) 713 410008
kulangwasos@gmail.com

HEBU vaa viatu vya daktari aliyeko ofisini akisubiri kuonana na wateja wake, yaani wagonjwa. Ghafla uko ofisini anaingia mgonjwa, unamkaribisha anakaa, lakini anaonekana anaumwa sana unamhoji, anakwambia kweli anajisikia vibaya.

Unaingiwa shaka kwamba pengine anajifanya tu kwa sababu saikolojia yako ya udaktari inakuonyesha kabisa haumwi ila ana lake jambo. Bila shaka huwezi kumfukuza wala kumkaripia, ila utampima ili kujiridhisha.

Kwa bahati mbaya matokeo yanasema haumwi chochote. We kama daktari na maadili yako, utakachofanya utampa pole na kumwambia ingawa vipimo havionyeshi chochote kibaya, pengine ni uchovu na anachotakiwa ni kurudi nyumbani apumzike na kunywa maji mengi hali itarejea kawaida.

Kama alikuwa anakudanganya akitarajia pengine atapata dawa akauzie wenzake, atakuwa amegonga mwamba na kurudi nyumbani mikono mitupu, lakini amepoteza muda na nguvu zake kutembea hadi hospitalini kujaribu kuhadaa.

Lakini kwa kuwa hana utaalamu, inawezekana pia bila shaka hali aliyokuwa anajisikia kuwa nayo, ilimfanya aamini kuwa anaumwa na hivyo kuamini kuwa matatizo yake yataishia hospitalini. Bahati mbaya kumbe haikuwa hivyo.

Haya mambo hutokea miongoni mwetu na wakati mwingine kushindwa kuaminiana na kudhani watu wanajifanya na yakikutana na madaktari wasiojali taaluma yao, ndio mtasikia alizidiwa baada ya kurudi kutoka hospitalini akapoteza maisha.

Kumbe daktari angekuwa makini hayo yasingemkuta mteja wake mpaka kupoteza maisha. Haya hutakuta pia katika maisha ya kawaida yasiyohusu magonjwa au ajali zingine zinazoweza kusababisha maafa katika jamii.

Ni hivi, Agosti mwaka huu mkoani Simiyu eneo la Lamadi wilayani Besega, wananchi waliandamana wakilalamikia upotevu wa watoto wakichukuliwa na watu wasiojulikana, wakielekea kituo cha Polisi kudai haki ya kusaidiwa.

Wananchi hao walikuwa wakilalamikia viongozi wa serikali wakiwamo ngazi ya ulinzi na usalama, ambako wamekuwa wakiwasilisha malalamiko yao ya kupotelewa watoto, lakini mara zote hakuna kinachofanyika, hivyo kupuuzwa na wao kuona wamechoka sasa wakitaka kujiridhisha kulikoni.

Lakini siku hiyo, polisi walikabiliana nao na kufyatua risasi iliyompata mmoja wa wananchi hao na kupoteza maisha, ni bahati mbaya sana kijana aliyepoteza maisha alikuwa ndiyo kwanza amemaliza kidato cha sita akijiandaa kujiunga na chuo kikuu.

Baada ya mambo kutulia, mwezi mmoja baadaye, viongozi wanapita vijijini kusikiliza kero za wananchi, lakini kwa maajabu, linaibuka suala la waliolalamikia watoto kutoweka, wakitakiwa kutoa uthibitisho wa madai yao mkutanoni.

Mmoja wa wakazi anasimama na kudai kuna kutoweka kwa baadhi ya watu na wengine kuumizwa, mwingine akidai kuwapo matukio ya mabaya zaidi, watoto kutekwa au kupotea na mabaya zaidi, wananchi kuishi kwa shaka na kujifungia majumbani kila ifikapo saa 12 jioni.

Pamoja na hayo, kadhia nyingine inayodaiwa kuwateka wakazi hao ni kasoro katika huduma nzuri ya kimatibabu katika baadhi ya maeneo, kukiripotiwa matukio dai la malipo kwa watoto wasiostahili kufanyiwa hivyo.

Kwani tayari ukiwa na kadi ya matibabu, hutakiwi kulipia, lakini unaweza kuiambulia dawa maumivu na zingine unajinunulia.

Kitendo cha wananchi hao kulalamika, kinamsababisha Mkuu wa Mkoa, kuwataka wathibitishe madai yao chini ya usimamizi wa polisi, huku akionya dhidi ya kutoa alichokiita taarifa za uongo, hivyo watu hao kupandishwa gari l kwenda kuthibitisha.

Kiongozi mkubwa anachukua kipaza sauti na kuhoji wananchi kama kweli kuna matukio hayo katika maeneo hayo na kujibiwa "hakunaaaa!" hata anapata nguvu ya kuwaweka chini ya ulinzi waliodai kuwapo matukio, hayo ili wakathibitishe.

Hivi kiongozi alitarajia majibu gani mbele ya Jeshi la Polisi? Alitarajia nini wakati mwezi mmoja tu kupita aliuawa mtu akiandamana? Kwani angefanya kama daktari alipomshauri mgonjwa akanywe maji mengi kutokana na uchovu ingekuwaje?

Kiongozi alichotakiwa kufanya ni kusikiliza malalamiko na baadaye angewaita kwa nafasi yake wananchi hao kuwahoji ofisini mwake, kwa utaratibu na pengine kama aligundua ni uongo basi wangemwambia kiini na angewaonya kuliko kuwakabidhi chini ya ulinzi.

Siku nyingine, kwa utaratibu huo wananchi wanaweza hata kubaini wahalifu kijijini kwao au wakielekea kwa Mkuu wa Mkoa na kunyamaza

kwani kusema kunaweza kuwasababisha waombwe uthibitisho.

Pia, kufanya hivi kutasababisha msuguano wa kuchukua sheria mkononi kimyakimya, wakiepuka kubanwa na Polisi kuthibitisha. Wanahofu, wakigoma kutoa taarifa wasiambiwe wanaficha wahalifu!

BIASHARA

UZALISHAJI WILAYANI UKIDIDIMIA...

# Mkuranga washtuka hujuma za korosho kukithiri kila kona zake

**Na Yasmine Protace,**
MKURANGA



Shangwe Twamara, Katibu Tawala Msaidizi wa Uchumi na Uzalishaji Mkoa wa Pwani, akiongea na wenyeviti wa vyama vya msingi wilayani Mkuranga. **PICHA: YASMINE PROTACE**

NI maandalizi ya msimu ujao wa korosho -2024/2025 ambao wakulima wengi wanatarajia kuinuka kiuchumi kupitia zao hilo.

Kumekuwapo na malalamiko mengi katika misimu tofauti ya korosho pale minada inapofanyika. Malalamiko mengi yanatajwa kutokea kwa wakulima, hasa minada inapofanyika na malengo hayafikiwi.

Hivi karibuni katika kikao kazi kilichowakutanisha wenyeviti wa vyama vya ushirika wilayani Mkuranga kujadili namna ya kusimama korosho, kuwaletea maendeleo wana Mkuranga, Meneja wa Chama cha Ushirika Mkoa wa Pwani, Hamis Mantawale, amekuwa na maoni yake.

Mantawale anasema ni wajibu wa vyama vya ushirika kuleta mabadiliko kwa wakulima wa zao hilo, huku akirejea namna wilaya ya Kibiti ilivyo na vyama vichache vya ushirika na bado inazalisha ufuta kwa wingi, ikifuatiwa na Rufiji na Mkuranga.

Anasema wilayani Mkuranga kunatuhumiwa kashfa ya kutorosha korosho, huku Rufiji na Kibiti kukibaki shwari kwa madai ya matukio hayo.

Meneja huyo wa Coreccu, anaongeza kutakuwapo kazi ya uhakiki, kila chama kunusuru mnada wa korosho na mbaguaji anatakiwa kufanya malipo kabla hajachukua korosho yake.

Katika msimu wa mwaka wa fedha 1924/25, tozo zote kimsingi zitalipwa na mnunuzi, huku mkulima atakachokifanya chini ya chama cha ushirika, ni kulipa shilingi mbili ya wadau na shilingi mbili ya 'primantcenter' na waraka wa Mrajisi Ushuru utakuwa shilingi 55.

Pia, anasema korosho ya Mkuranga ziko chache kutokana na baadhi yao wakulima hawayatunzi mashamba, huku wengine wakiyatelekeza.

Ofisa Kilimo Mwandamizi wa Bodi ya Korosho, Tawi la Dar es Salaam, Abraham Fredrick, anasema korosho zilizo chini ya ubora 'Daraja 35', zinatakiwa kuteketezwa.

" Kama korosho hizo mtaanzia huku zikiwa zimeshuka ubora, mjue mnatengeneza mazingira mabaya katika msimu ujao wa korosho," anasema.

Shangwe Twamala, Katibu Tawala Msaidizi Uchumi Mkoa wa Pwani, anasema Mkuranga kupitia vyama vya ushirika, kunatakiwa kuletwa mabadiliko kupitia zao hilo.

Anasema ushirika kila mahali duniani kunaweza 'kumtoa mtu' katika hali duni na kumpeleka katika Uchumi na Mkuranga kupitia vyama vya ushirika, vinatakiwa vilete mabadiliko, hivyo vinatakiwa kuhakikisha mazao yana ubora.

Twamala anasema, mkoa wa Pwani una mazao matatu ya biashara na sasa limeongezeka alizeti, akifafanua: "Ulikuwa na mazao matatu ya biashara, ambayo ni mbaazi, korosho, ufuta sasa limeongezeka zao la alizeti.'

Anasema katika msimu wa mwaka 2025/26 wanatarajia kukusanya tani 36,000 za korosho mkoani Pwani, akifafanua katika mwaka wa fedha 2023/24, korosho mkoani Pwani walikusanya tani 22,000.

Mussa Mng'eresa, Mwenyekiti wa Correcu Mkoa wa Pwani, anaiomba serikali iwasaidie kila inapofika msimu wa mavuno ya korosho, kuwapo dirisha la benki wanaletewa na sio kukaa foleni ilivyo sasa.

Anawataka viongozi wa ushirika mahali hapo wasimamie zao la korosho kuinua uchumi wa wakulima, akiwataka kusifanyike udanganyifu na kila chama kihakikishe kinaweka korosho katika magunia yenye nembo.

Mng'eresa anasema, uamuzi uliofikiwa ni kwamba hakutaruhusiwa chama chochote kubeba korosho ambazo magunia yake hayana nembo.

Kuliripotiwa kwamba Mkuu wa Mkoa Pwani, Aboubakari Kunenge, alitarajiwa kuwapo wilayani Mkuranga wiki hii, kufuatilia jambo hilo, hata hivyo ziara hiyo imeahirishwa.

## Marufuku ya Samia 2021, nchi kung'aa kimataifa na ukakasi wake

**INATOKA UK.11**

**ATHARI ZA RUSHWA**

Akizungumza na Nipashe, Emmanuel Lewis, mkazi wa Dodoma anashauri ni muhimu kwa serikali na jamii kuchukua hatua madhubuti kupambana na rushwa na kuboresha mfumo huo, kuhakikisha haki ya kodi inatekelezwa kwa usawa na ufanisi, ili kuleta matokeo chanya kwa jamii na kuimarisha maendeleo yao.

Lewis anafafanua kwamba rushwa inadhuru ukuaji uchumi, kwa kuzuia uwekezaji wa ndani na kigeni kwa sababu wawekezaji wanahitaji mazingira safi ya biashara bila vitendo vya rushwa, akisema kukosekana haki ya kodi kunawakatisha tamaa, mifumo duni ya usimamizi wa kodi huongeza nafasi ya ufisadi, serikali inatakiwa kuimarisha mifumo yake kuzuia rushwa.

"Rushwa inakwamisha uwezo wa serikali kutoa huduma bora zinazotegemea mapato ya kodi, wananchi wanapolipa kodi lakini wanakosa huduma za msingi kama elimu na afya bora, wanashindwa kuona umuhimu wa kulipa kodi," anasema.

Elizabeth Faustine kutoka Mwanza, anaeleza rushwa inarudisha nyuma maendeleo, maana mfanyabiashara anapotoa rushwa 'kurahisishiwa maisha' inaikosesha serikali mapato.

Vitalis Dahaye, anasema chanzo kingine ni wananchi kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu wajibu wao wa kulipa kodi, pia umuhimu wake, hata inawarahisishia watumishi wa umma wapotofu kutumia elimu duni ya wananchi kujinufaisha kwa rushwa.

Anataja chanzo kingine ni mamlaka zinazodhibiti rushwa kulegalega, katika udhibiti.

**WASOMI WAFUNGUKA**

Mtaalamu wa Uchumi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Prof. Abel Kinyondo, anaeleza kuwa uwajibikaji ni nguzo muhimu ya kudhibiti mambo mbalimbali ikiwamo rushwa, ukwepaji kodi na utoroshaji fedha.

Anasema, ili kujinasua kunahitajika kutumika malighafi zinazopatikana nchini, viongozi kuwa mbali na maslahi binafsi, wawekezaji kutokutumia njia za udanganyifu kukwepa kodi au kulipa kidogo na wananchi kutokulichukulia suala la ulipaji kodi ni hiyari.

Pia, anaeleza umuhimu wa kuwapo mabadilishano ya taarifa kutoka nchi moja kwenda nyingine ni jambo la muhimu na lenye maslahi mapana ya nchi.

Aidha, katika utoroshwaji fedha, Prof.Kinyondo ameweka wazi kuna vyanzo vikuu vitatu visivyo halali kwa mapato, usafirishaji haramu wa fedha na matumizi haramu ya fedha mfano kuwezesha matukio ya kigaidi.

**NENO LA TRA**

Kwa mujibu wa Taarifa ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ya Kodi na Ushuru 2023 /2024 inaweka wazi umuhimu wa kulipa kodi na adhabu zinazoutolewa.

Pia, inataja kusajili wafanyabiashara wadogo na watoa huduma kwenye sekta isiyo rasmi watatambuliwa na kupewa vitambulisho, wenye mauzo ghafi yasiyozidi Sh. milioni nne kwa mwaka nao hawatalipa kodi.

Taarifa inafafanua, mauzo ghafi kwa mwaka yanapozidi Sh. milioni 100, wauzaji watawajibika kutengeneza hesabu za mizania, huku mtu binafsi mwenye mauzo ghafi kwa mwaka kuanzia Sh.milioni 11 anatakiwa kutoa risiti za kielektroniki.

Aidha, inafafanuliwa mlipakodi mwenye mauzo ghafi chini ya Sh.milioni 11 anatakiwa kutoa risiti ya kuandikwa kwa mkono zenye jina la muuzaji,TIN yake, jina la mnunuzi, aina ya bidhaa na thamani yake.

Taarifa hiyo inaongeza kuwa muuzaji atakayeshindwa kutoa risiti ama akatoa risiti yenye thamani ya uongo atalipa faini ya kiasi kikubwa kati ya asilimia 20 ya thamani ya bidhaa au huduma ama kulipa shilingi milioni 1.5, huku mnunuzi asiyedai risiti atalipa faini ya kiasi kikubwa kati ya asilimia 20 ya kodi iliyokwepwa.





# NBAA: Matumizi teknolojia yaipaisha Tanzania kimataifa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKURUGENZI Mtendaji wa Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu nchini (NBAA), Pius Maneno, ametaja vigezo vinavyoifanya Tanzania kushika nafasi nzuri katika masuala ya utawala na usimamizi wa hesabu za serikali Afrika.

Alitaja vigezo hivyo kuwa ni kutoa ripoti ya ukaguzi wa hesabu za serikali kwa wakati, kufuata miongozo yake kwa umakini na matumizi ya teknolojia.

Alisema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua semina ya wakaguzi wa serikali iliyolenga kujadili viwango vya ukaguzi na kujengeana uwezo.

"Madhumuni ya mafunzo haya ni kuelimishana kutumia viwango vizuri vya ukaguzi na utayarishaji fedha ili nchi yetu iendelee kusonga mbele na kutunza mali ya umma kama inavyotarajiwa," alisema.

Msaidizi wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Isaya Jeremiah, alisema mafunzo hayo ni muhimu na yanalenga kuleta ufanisi kwa watumishi na kutambua mambo mapya yaliyojitokeza kwenye taaluma ya uhasibu.

Kadhalika, alisema mafunzo hayo yatasaidia kuboresha ukaguzi wao na kumwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuendelea kutoa ripoti zenye viwango.



Wananchi wa Kijiji cha Muhintiri, wilayani Ikungi, mkoani Singida, wakishiriki maziko ya kijana, Frank Joseph Mnyaru (28) kijijini hapo mapema wiki hii, anayedaiwa kuuawa na askari mgambo kwa kumwingizia mti sehemu ya haja kubwa katika ofisi ya Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Ugonjwa wa moyo wazidi kuwatesa vijana

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa ugonjwa wa moyo hapa nchini umeathiri kwa kiwango kikubwa vijana kuanzia umri wa miaka 30 hadi 45, tofauti na mataifa ya Ulaya ambapo tatizo hilo huwapata watu wenye umri wa miaka 50 hadi 60.

Kutokana na hali hiyo, madaktari bingwa wa upasuaji wa moyo kutoka Uholanzi wameweka kambi ya matibabu katika Hospitali ya Benjamin Mkapa na kutoa msaada wa vifaa vya matibabu ya moyo vyenye thamani ya Sh.milioni 400.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dodoma kuhusu ujio wa madaktari hao, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Prof. Abel Makubi, alisema moja ya sababu inayochangia hali hiyo ni ugumu wa maisha na mtindo wa kula.

"Moja ya tabia ambazo vijana wanakuwa wagumu kubadilika ni pamoja ulaji wa vyakula, uvutaji sigara, ulaji wa chumvi nyingi, pamoja na kushindwa kufanya mazoezi," alisema.

Alisema jamii inapaswa kubadilika ikiwamo kufuata taratibu zinazotolewa na wataalamu wa afya ili kupunguza tatizo la moyo.

"Tunashukuru tiba inatolewa lakini jamii inajaribu kujikinga na tatizo hili kwa kubadilisha mfumo wa ulaji wa vyakula," alisema Prof. Makubi.

Hata hivyo alitoa rai kwa wakazi wa jijini Dodoma na mikoa jirani kutumia hospitali hiyo kwa ajili kupata matibabu ya ugonjwa huo.

"Hadi sasa tayari tumewafanyia upasuaji wagonjwa wenye matatizo ya moyo zaidi ya 40, lakini pia wamefanyia uchunguzi wagonjwa 3,000 na wagonjwa 500 wamezibuliwa mishipa," alisema.

Kuhusu vifaa vya matibabu ya moyo vilivyotolewa, Dk. Makubi alisema vitasaidia kwa kiasi kikubwa kutokana na matibabu ya moyo kuwa na gharama kubwa.

Daktari bingwa wa upasuaji wa moyo kutoka Uholanzi, Dk. Grandjean Gerhard Jan, alisema wataendelea kushirikiana na BMH katika utoaji wa matibabu ya moyo kwa wagonjwa mbalimbali.

Hivyo, aliishukuru Serikali ya Tanzania kutokana na uwekezaji wanaofanya katika sekta ya afya.

Daktari bingwa wa upasuaji moyo na mishipa, Dk. Ahmed Toure, alisema kutokana na uwapo wa tatizo hilo zinahitajika hospitali zaidi ya 25 kwa ajili ya utoaji wa matibabu ya moyo.

## Halmashauri Itigi yawaita vijana kuchukua mamilioni

**Na Thobias Mwanakatwe,** ITIGI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Itigi mkoani Singida imetoa wito kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kuchangamkia fursa ya mikopo ambapo Sh.milioni 442.7 zimetengwa kwa ajili ya kutoa mikopo.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Ayoub Kambi, akizungumza juzi na vikundi vya wajasiriamali, wazee wa kimila, wazee, watumishi na wananchi, alisema fedha hizo zilianza kutengwa katika robo ya kwanza ya Julai-Septemba ya mwaka wa fedha 2024/25.

Kambi alisema vikundi vinavyotakiwa kuomba mikopo ni kile ambacho kinatambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi na halmashauri, kinachojishughulisha na shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati au kikundi kinachotarajia kuanzisha shughuli za ujasiriamali.

Alisema sifa nyingine kwa kikundi cha wanawake na vijana lazima kiwe na idadi ya wanakikundi kuanzia watano na kuendelea na kikundi cha watu wenye ulemavu kiwe na wanakikundi wasiopungua wawili.

"Kwa kuzingatia Kanuni ya 7 (1) mtu mwenye ulemavu anaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha watu wenye ulemavu endapo timu ya menejimenti ya halmashauri itajiridhisha kuwa amekosa mtu mwingine mwenye ulemavu wa kuungana naye katika eneo lake," alisema.

Alisema sifa zingine ni kikundi kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiujasiriamali na wanakikundi lazima wawe ni raia wa Tanzania wasio na ajira rasmi, wenye na akili timamu na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea. Kadhalika alisema kikundi kinachoomba mkopo kinapaswa kuwa na viambatisho ambavyo ni barua ya kuomba mkopo iliyopitishwa na Ofisa Mtendaji wa Kijiji, muhtasari wa kikundi wa kuomba mkopo, andiko la mradi unaoombewa mkopo kwa kuzingatia fomu iliyo ndani ya mfumo na taarifa ya akaunti ya benki.

# Kichaa cha mbwa kinaua watu 59,000 kila mwaka

**Na Mwandishi Wetu**

KILA mwaka watu 59,000 duniani wanafariki dunia kutokana na ugonjwa wa kichaa cha mbwa, huku ugonjwa huo ukitajwa kuwa ni tishio nchini husuani katika jamii zenye uelewa mdogo na upatikanaji hafifu wa huduma za mifugo.

Kutokana na hali hiyo, Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) kupitia mradi wa Breakthrough Action, kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania wameamua kuungana katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo.

Akizungumza wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kichaa cha Mbwa, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Abdul Mhinte, alisisitiza umuhimu wa elimu kwa jamii na mikakati ya chanjo katika kupambana na ugonjwa huo.

Pia, alihimiza kuimarishwa kwa ushirikiano kati ya maofisa wa afya ya umma na jamii za mitaa ili kuimarisha mwitikio wa pamoja.

"Kichaa cha mbwa kinaweza kuzuilika. Lengo letu ni kuhakikisha kila mbwa nchini anapatiwa chanjo na kila mwananchi anajua cha kufanya endapo atang'atwa na mbwa. Kila jamii inapaswa kuchukua jukumu lake katika vita hivi," alisema.

Alisema kampeni ya "Holela-Holela Itakukosti," ambayo tafsiri yake ni "uzembe ni gharama," ilichukua nafasi kubwa katika kuongeza uelewa kuhusu ugonjwa wa kichaa cha mbwa.

Mhinte alisema lengo la kampeni hiyo ni kuiwezesha jamii kupambana na ugonjwa wa kichaa cha mbwa, kwamba USAID na Tanzania inawakumbusha wananchi kuwajibika na kuondoa vikwazo ili kushinda vita dhidi ya ugonjwa huo.

Baadhi ya wananchi wakielezea kampeni hiyo akiwamo Revina ambaye ni mama wa watoto watatu kutoka Mwanza, alisema: "Kabla ya kampeni, sikuwa najua hatari ya kichaa cha mbwa. Tulipojifunza kuwa mbwa wetu wanapaswa kuchanjwa, tulichukua hatua mara moja. Sasa, nina amani kuwaacha watoto wangu kucheza nje."

Alisema kampeni ya Holela-Holela pia inalenga kupambana na sababu zote zinazochangia kuwapo kwa ugonjwa huo kama vile uelewa mdogo, juhudi hafifu za chanjo na usimamizi usio salama wa wanyama.



# Wabeba wagonjwa, wajawazito kwa machela kusaka matibabu

**Na Nebart Msokwa,** TUKUYU

ZAIDI ya wakazi 7,000 wa Kata ya Masoko Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, wanatarajia kuondokana na adha ya kutembea umbali mrefu na kubeba wagonjwa kwenye machela kwenda kupata matibabu hospitalini baada ya serikali kuwajengea kituo cha afya.

Imefahamika kuwa wakazi hao wamekuwa wakipata matibabu kwenye vituo vya afya vya kata zilizoko jirani na Hospitali ya Wilaya ya Rungwe Makandana iliyopo mjini hapa.

Wakazi hao wamekuwa wakilazimika kusafiri na kusafirisha wagonjwa kwa kuwabeba kwenye machela umbali wa zaidi ya kilomita 18 hadi zahanati ya Kalebela na Hospitali ya Makandana kupata matibabu.

Waliyasema hayo juzi baada ya Waziri wa Katiba na Sheria, Profesa Paramagamba Kabudi kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa Kituo cha Afya Masoko ambao uko mbioni kukamilika.

Mmoja wa wakazi hao, Mariam Mwakalinga, alisema kitendo cha wagonjwa kubebwa kwenye machela na kusafirishwa umbali mrefu, kimekuwa kikihatarisha maisha yao kutokana na eneo lao kuwa na milima.

Mariam, alisema baadhi ya wajawazito wanaosafirishwa kwa machela, wamekuwa wakijifungulia njiani, wengine kufa pamoja na watoto wao.

"Mabinti zetu walianza hata kuogopa kuzaa kwa sababu ya mazingira yaliyoko, ukitaka kukodi hata pikipiki ya kumsafirisha mgonjwa kwenda huko Kalebela au Makandana gharama yake ni kuanzia Sh. 50,000, wengi tumekuwa tukishindwa kuimudu," alisema Mariam.

**kwenda huko Kalebela au Makandana gharama yake ni kuanzia Sh. 50,000, wengi tumekuwa tukishindwa kuimudu," alisema Mariam.**

Tulinagwe Kanyamale, alishukuru serikali kwa kuwasogezea huduma hiyo kwa kuwa itawasaidia kupunguza gharama za matibabu na muda wa kusafiri kwenda kupata maeneo ya mbali.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Renatus Mchau, alisema serikali ilitoa Sh. milioni 800 kati ya hizo, Sh. milioni 500 ni kwa ujenzi wa kituo hicho na Sh. milioni 300 ununuzi wa vifaa tiba.

Mchau, alisema ujenzi wa kituo hicho unafanyika kwa kutumia akaunti ya dharura 'Force Account'.

Alisema kufikia mwishoni mwa mwezi ujao, ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje utakuwa umekamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

"Wananchi wamekipokea kituo hiki kwa moyo na wanashiriki kwenye ujenzi, lengo letu kabla ya Januari mwakani baadhi ya huduma zianze kutolewa hapa na kuwapunguzia adha ya kutembea umbali mrefu," alisema Mhau.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema serikali imetoa fedha nyingi kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika wilaya hiyo, ikiwamo ujenzi wa vituo vya afya, elimu, miundombinu ya barabara na kilimo.

Kwa upande wake, Prof. Kabudi aliiagiza halmashauri ya wilaya hiyo kuhakikisha ujenzi wa kituo hicho unakamilika na kuanza kutoka huduma Desemba mwaka huu ili kuwaondolea wakazi hao mazingira magumu wanapohitaji matibabu.

Alimtaka mkurugenzi huyo kupiga kambi katika eneo hilo na kuhakikisha ujenzi wa majengo yote muhimu unakamilika kwa wakati.

Kabudi yuko mkoani Mbeya kwa ziara ya kikazi, anatarajiwa kutembelea halmashauri zote, kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kufungua na kuzungumza na wananchi katika mikutano ya hadhara.



Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Paramagamba Kabudi (kulia), akikagua ujenzi wa Barabara ya Ndulilo-Itete, wilayani Rungwe, mkoani Mbeya juzi, yenye urefu wa Km. 11.35 inayojengwa na serikali kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 8.9, alipokuwa kwenye ziara wilayani humo. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Jaffar Haniu. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Vijana, wanawake, wenye ulemavu kukopeshwa bil. 2.7/-

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

HALMASHAURI ya Mji wa Njombe mkoani hapa imetenga zaidi ya Sh. bilioni 2.7 kukopesha vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kwa ajili ya kuanzisha miradi ya ujasiriamali na kuondokana na umaskini.

Hayo yalielezwa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa wakati mafunzo kwa wataalamu kuanzia ngazi za kata kwa ajili ya kwenda kutoa elimu kwa wanufaika wa mikopo hiyo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri nchini.

Kasongwa, alisema kuwa: "Wakati tumeambiwa tusubiri tusikopeshe kweli mlisubiri, hizi hela hazikuguswa zilibaki kama zilivyo ili kusubiri melekezo," alisema Kasongwa.

Alisema kurejeshwa kwa mikopo hiyo ni fursa kwa wananchi kwa sababu kwa sasa itatolewa hata kama kila mmoja kwenye kikundi ana biashara yake.

Alionya kuwa uongo na kukosa uaminifu kwa vijana katika mikopo hiyo, kunarudisha nyuma na kukwamisha jitihada za kujiletea maendeleo, hivyo wanapaswa kubadilika.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Kuruthum Sadick, alisema maofisa maendeleo ya jamii wanapatiwa mafunzo ili waende kuhamasisha vikundi na kuvisajili.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri hiyo, Enembora Lema, alisema watakwenda kutoa elimu mtaa kwa mtaa na kijiji kwa kijiji ili wananchi waweze kujitokeza kuchangamkia fursa hiyo.

Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Mkoa wa Njombe, Samwel Mgaya, aliwataka vijana kutumia mikopo hiyo kujiletea maendeleo na kukuza uchumi wao.

Baadhi ya wakazi mjini Njombe akiwamo Benjamini Mwenda, alisema kurejeshwa kwa mikopo hiyo kutasaidia kufufua matumaini mapya baada ya sababu zao kusimamishwa mwaka jana kuanza upya.

"Tunaishukuru serikali kwa kuturudishia mikopo hii kwa sababu ilikuwa inatusaidia na wataalamu wazingatie mikopo hii iende sehemu sahihi," alisema Mwenda.

# Wachimba madini wapata viongozi

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

ISACK Ngelangela, amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Wachimbaji Wadogo na Wakati wa Madini Mkoa wa Ruvuma (RUVREMA) kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Akitangaza matokeo juzi kwenye Mkutano Mkuu wa chama hicho, Msimamizi wa Uchaguzi huo, Alfred Luvanda, aliwataja wengine waliochaguliwa kuwa ni Kassimu Pazi (makamu mwenyekiti), Johnbosco Mvula (Katibu), Christopher Simkoko (mweka hazina) na wajumbe watano wa kamati ya utendaji.

Luvanda ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Wachimba Madini Wazawa nchini (FEMATA), aliwahimiza wachimbaji ambao bado hawajajiunga waone umuhimu wa kujiunga na vyama hivyo kwa kuwa serikali iko tayari kuwasaidia kupata soko tofauti na miaka ya nyuma.

"Kukosa soko la uhakika lilikuwa ni jambo ambalo linasababisha wengi wao kuuza madini kwa walanguzi kwa bei ndogo ambayo hailingani na thamani," alisema.

Aliwaasa viongozi hao waliochaguliwa kuwa karibu na wanachama wao, kusikiliza kero, kuwasaidia na kuwaelekeza sehemu sahihi ya kuuza madini kwa bei kubwa na kupata faida.

Akizungumza baada ya kutangazwa mshindi, Ngelangela, alisema serikali imeleta mabadiliko katika sekta ya madini ili wachimbaji kupata faida na kuchangia mapato kwa kulipa kodi.

"Madini yalikuwa yanauzwa bila kufuata taratibu, kwa sasa wachimbaji wadogo na wa kati wanapofanikiwa kupata madini, wanafahamu mahali pa kwenda kuyauza ambako serikali imetenga kwa ajili ya masoko ya madini," alisema.

Aliiomba serikali kupeleka majisafi na salama kwenye maeneo ya wachimbaji hao ili waweze kupata huduma hiyo ili kuwanusuru na magonjwa ya milipuko kwa kutumia maji machafu.

Kwa mujibu wa Ngelangela, Ruvuma kuna madini mengi, yakiwamo makaa ya mawe, dhahabu, ulanga na vito.



# Mwigulu: CISNA simamieni usalama, mifumo ya fedha

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, amesema Mamlaka ya Usimamizi wa Bima, Masoko ya Mitaji na Huduma za Kifedha, zisizo za Kibenki (CISNA) ni jukwaa sahihi la kubadilishana uzoefu na utaalamu.

Alisema hayo juzi Zanzibar wakati akifungua Mkutano wa 47 wa mwaka wa Kamati ya CISNA chini ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC). Hotuba ya Dk. Mwigulu ilisomwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu, Ali Suleiman Mrembo, ambaye alisema CISNA inatakiwa kuunga mkono juhudi za kuimarisha mazingira ya usimamizi wa biashara miongoni mwa nchi wanachama.

Alisema pia inatakiwa kubadilishana taarifa ili kuzuia uhalifu, kusimamia maslahi ya wadau na kuimarisha usalama wa mifumo ya kifedha katika eneo la SADC.

Mrembo alisema katika maeneo mengine ya dunia, Kanda ya SADC imekumbana na madhara yanayotokana na ugonjwa wa corona, mivutano ya kikanda iliyotokana na mzozo kati ya Urusi na Ukraine, migogoro ya Mashariki ya Kati na sasa ukame mkali katika nchi za Kusini mwa Afrika.

Alisema Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) linatabiri mwelekeo chanya wa ukuaji wa uchumi wa nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara ukiwa na ongezeko la wastani wa ukuaji wa pato la taifa kutoka asilimia 3.4 mwaka 2023 hadi asilimia 3.8 mwaka 2024, huku nchi nyingi zikitarajiwa kuwa na ukuaji zaidi ya wastani.

Aidha, alisema ili kudumisha mwenendo chanya wa kiuchumi katika ukanda huo, kunahitajika juhudi za pamoja kutoka kwa wadau na baadhi ya hatua muhimu katika kuharakisha ukuaji wa kiuchumi wa kanda.

**Alitaja hatua hizo ni pamoja na kutekeleza mikakati ya kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi, kuendeleza utekelezaji wa malengo ya huduma jumuishi za kifedha na kusaidia...**

Alitaja hatua hizo ni pamoja na kutekeleza mikakati ya kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi, kuendeleza utekelezaji wa malengo ya huduma jumuishi za kifedha na kusaidia maendeleo ya biashara chanya na za kibunifu.

Kadhalika alisema majanga yanayohusiana na hali ya hewa na mabadiliko ya tabianchi yanazidi kuwa ya mara kwa mara na makali kadri joto la dunia linavyoongezeka.

Waziri huyo alisema mabadiliko ya tabianchi yanaweka changamoto nyingi katika jamii, yakihusisha mifumo ya ikolojia, uchumi, jamii na ustawi wa binadamu.

Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Emmanuel Tutuba, alisema kuwa jukumu kuu la CISNA ni kuoanisha kanuni na miundo ya usimamizi ya nchi wanachama na kuhakikisha kuwa zinakidhi viwango vya kimataifa vilivyowekwa na taasisi za viwango za kimataifa.

Mwenyekiti wa CISNA, Keneth Matomola, alisema lengo la mkutano huo ni kujadili mambo yanayohusu jumuiya hiyo katika kufikia maendeleo yake kwa vile wajumbe wa jumuiya hiyo wanaundwa kutoka nchi mbalimbali za SADC.

Alisema mkutano huo utakuwa fursa ya kujadili wasuala ya mabadiliko ya tabianchi ambapo hivi sasa changamoto kubwa imeonekana katika nchi wanachama na dunia kwa ujumla.



Kamishna wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar, Kanali Burhani Zuberi Nassoro (mwenye sare ya jeshi), akimwaga mafuta ya taa katika zoezi la uteketezaji wa kilo 180 za dawa mbalimbali za kulevya katika eneo la Kwareni Pemba, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dawa za kulevya kilo 180 zateketezwa

**Na Mwandishi Wetu,**
PEMBA

DAWA za kulevya kilo 180 za aina mbalimbali ikiwamo bangi, heroin, cocain, cideibe, afyuni na mirungi zimeteketezwa visiwani Zanzibar.

Dawa hizo ziliteketezwa juzi na kamati ya kuteketeza dawa za kulevya eneo la Kwareni Wilaya ya Chakechake Zanzibar, ikiongozwa na viongozi na wajumbe wa kamati hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uteketezaji wa dawa hizo, Katibu Mkuu Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Maryam Abdallah Sadala, alisema dawa hizo ni hatari kwa matumizi ya binadamu na zimekuwa zikiwaathiri vijana.

Pia, aliipongeza Tume ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar, katika kuhakikisha inazikamata na kuziteketeza dawa hizo kwa ajili ya kuinusuru jamii.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Mgeni Jailani Jecha, alisema zoezi hilo limeenda vizuri na wamefanikiwa kuzihakiki na kuziteketeza dawa hizo.

Mgeni ambaye ni Mkurugenzi wa Mashtaka alisema serikali imeweka nia ya kupambana na dawa za kulevya kwa sababu zimekuwa hatari kwa maisha ya wananchi.

Kamishna wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar, Kanali Burhani Zuberi Nassor, alisema katika uteketezaji huo ulihusisha bangi kilo 127, Heroin (43), mirungi (71) na mofyum (6).

Kanali Burhan alisema dawa hizo zisipotetezwa zinaweza kurudi mitaani na kuathiri watoto.

Aidha, aliwasisitiza wananchi kuendelea kutoa ushirikiano na taasisi husika pamoja na kuwafichua wote wanaojihusisha na biashara hiyo.

Alisema serikali imedhamiria kuhakikisha inatokomeza dawa za kulevya nchini na kuwatahadharisha wafanyabiashara wa dawa za kulevya kuacha.

# ZRA yavunja rekodi ukusanyaji mapato

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Mapato Zanzibar (ZRA) imevuka lengo la ukusanyaji mapato kipindi cha Septemba kwa kukusanya Sh. bilioni 76.497, matarajia yalikuwa kukusanya Sh. bilioni 74.

Kaimu Mkurugenzi wa ZRA, Said Ali Muhamed, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari, akisema ongezeko hilo ni ufanisi wa asilimia 103.31 wa makusanyo ya mapato yaliyotarajiwa.

Alisema makusanyo halisi ya kipindi cha Septemba 2023/2024, yalikuwa ni Sh. bilioni 61.694, ambayo yakilinganishwa na makusanyo halisi ya Septemba mwaka huu yanaonesha ukuaji wa makusanyo halisi wa asilimia 23.99.

Kadhalika, alisema katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2024/2025, ZRA ilikadiriwa kukusanya Sh. bilioni 194.031 na imefanikiwa kukusanya Sh. bilioni 200.934, ambao ni ufanisi wa asilimia 103.56 wa makusanyo ya mapato yaliyotarajiwa.

"Kwa kulinganisha na makusanyo halisi ya robo ya kwanza ya mwaka uliopita wa 2023/2024, yalikuwa ni Sh. bilioni 161.831, ambayo yakilinganishwa na makusanyo halisi ya robo ya kwanza ya mwaka huu wa fedha wa 2024/2025, yanaonesha ukuaji wa makusanyo halisi wa asilimia 24.16," alisema.

Akizungumzia ufikiaji wa lengo la makusanyo ya kodi kwa asilimia 103.56, pamoja na mambo mengine alisema, umesababishwa kuimarika na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi kati ya Zanzibar na Tanzania Bara, zinazotokana na sera na uongozi wa Dk. Samia zilizoimarisha mazingira ya biashara.

Alisema sababu zingine ni kuendelea kuimarisha uhusiano mzuri na walipakodi ikiwemo kusaidia kurahisisha biashara zao pamoja na kuwafikia na kuwasilikiliza walipakodi kupitia njia mbalimbali ikiwemo kuwatembelea na kwa kutumia Kituo cha Mawasiliano kwa Walipakodi cha ZRA.

Alitaja nyingine ni programu ya kupokea maoni ya funguka kulikosababisha kuongezeka kwa ulipaji kodi wa hiari.

"Pia kuimarika kwa matumizi sahihi ya mifumo katika usimamizi wa kodi ikiwemo matumizi ya mashine ya risiti za kielektroniki na matumizi ya mfumo wa ukusanyaji wa mapato sambamba na kuongezeka kwa utoaji wa elimu ya kodi kupitia njia mbalimbali," alisema.

Hata hivyo alisema kuongezeka kwa ufuatiliaji wa karibu wa walipakodi kulikotokana na kuongeza idadi ya watumishi (wa ajira ya muda) wa mamlaka kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za kikodi kwa walipakodi na jamii.

Alisema utekelezaji wa marekebisho ya sheria za kodi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 nao umechangia hatua ambayo imesababisha kuimarika kwa ukusanyaji katika vianzio vya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), ushuru wa bidhaa, ada za bandari na kodi ya miundombinu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SIMON FRANK MARTIN** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 602 BEL – MITSUBISHI PAJERO** yenye Chassis namba **JMYLRV96W9J000405**. Engine namba **4M40HL5063.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/213768/2024.**



### AFFIDAVIT OF ONE AND THE SAME PERSON

**CHANDE JUMA ABDALLAH** of P.O. Box ..............**DAR ES SALAAM** adult Muslim solemnly state as follows;

- That Iam the deponent herein hence conversant with the facts Iam about to depose.
- That I know by fact, I by the name **CHANDE JUMA ABDALLAH** appearing in my both certificate and National Identification Card refer to one and the same person as **JUMA CHANDE ABDALLAH** and **ANDREW JOHN LWANDA** appearing in my academic certificate and marriage certificates respectively.
- That the forenamed names of **CHANDE JUMA ABDALLAH, JUMA CHANDE ABDALLAH** and **ANDREW JOHN LWANDA** refer to one and the same person.
- That the above is the variations of the same name and should not be considered name changes.
- I execute this Affidavit to the truth of the foregoing facts and for whatever legal purpose that this Affidavit may serve.
- That all what is stated under paraghaph 1,2,3,4,5,6 are true to the best of my knowledge and beliefs.

**KATIKA BARAZA LA ARDI NA NYUMBA WILAYA YA MBARALI**
**LILILOPO RUJEWA**
**MAOMBI NA. 91 MWAKA 2023**
**MLETA MAOMBI HUSSEIN M. WAMELI**
**DHIDI YA**
**MJIBU MAOMBI GISENA MPONEJA**
**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA: GISENA MPONEJA**

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kutajwa tarehe 18 Mwezi 10 Mwaka 2024 saa 2:00 asubuhi mbele ya Mh. A. MAPUNDA Mwenyekiti wa baraza. Hivyo unaamriwa mbele ya baraza siku hiyo bila kukosa.

Fahamu kwamba unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi/majibu ya rufaa ndani ya siku ishirini na moja au na kiapo kinzani ndani ya siku saba (7).

Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/mhuri wa baraza hii leo tarehe 03 Mwezi 10 Mwaka 2024.

MWENYEKITI WA BARAZA

**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT**
**(CAP 117)**
**CHANGE OF NAME BY DEED POLL**

**THIS CHANGE OF NAME DEED i**s made this 20th day of August, 2024 by me BAHATI PETER MWALUSAKO formerly known as BAHATI KENNEDY KOROSSO, of P.O. Box 281 KYELA a resident of KYELA TOWN.

WITNESS AND IT IS HEREBY DECLARED as follows:

- FOR THE PURPOSE of evidence of such determination, I do hereby declare, that my child shall at all times herein in all records, deeds, documents and other writings and in all action, suits proceedings as well as public and private dealings transaction and occasions whatsoever use and subscribe the said name of BAHATI PETER MWALUSAKO as her name in lieu of substitution for my former name of BAHATI KENNEDY KOROSSO.
- AND IN PURSUANCE of such change of name(s) as aforesaid I DECLARE I shall at all time hereafter in all records, documents and other writings and in all actions and dealings and on all occasions whatsoever use the new names of BAHATI PETER MWALUSAKO in substitution for my former names of BAHATI KENNEDY KOROSO.
- AND I HEREBY AUTHORIZED AND REQUIRE all persons at all times to describe and address me by the new names of BAHATI PETER MWALUSAKO, and have affixed my signature my signature the day and year herein written.

Dated at Mbeya this 20th Day of August, 2024.

Dated at Mbeya this 20th Day of August 2024

Signed and delivered at Mbeya.
By the said **Bahati Peter Mwalusako**
Who is known to me personally in my
Presence this 20th day of August 2024

B. Mwalusako
DEPONENT



Before me
Name: Ezekiel ...
Signature ......
Postal Address......
Qualification: commissioner for oath

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **ELIAMINI KHAMISI MOHAMEDI** anatangaza kupotea kwa kadi ya pilipiki aina ya SAN LG yenye namba za usajili MC 203 CGW. Kwa yeyote atakayeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu. Amefika Polisi na amepewa Loss Report. Taarifa Polisi: **PHQ/TAN/TAN/10706/2024.**

**IN THE DISTRICT COURT OF KYELA**
**AT KYELA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 24288 OF 2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE MANENO NYANYILE BUKUKU**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY OSIANA NYANYILE BUKUKU**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

**ALL PERSON** claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 25th of October, 2024.

Dated at **KYELA** this 30th day of September, 2024.

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
KYELA.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**
**IDARA YA UHAMIAJI**
**TAARIFA IMETOLEWA KWAMBA:**



**JUDITH FLORA ETABALE WANDA**
**S.L.P 307**
**MWANZA**

AMBAYE PICHA YAKE IMEBANDIKWA HAPO JUU.
ANAOMBA URAIA WA TANZANIA KWA WAZIRI WA MAMBO YA NDANI
UTAIFA WAKE KWA SASA NI KENYA, NCHI ATOKAYO NI KENYA.
SHUGHULI ZAKE NI MWALIMU WA CHUO KIKUU CHA ST. AUGUSTINE MWANZA
ANUANI YA MUAJIRI WAKE NI S.L.P 307 MWANZA
AMEISHI HAPA NCHINI TANGU 2016.
MTU YEYOTE ALIYE NA SABABU ZOZOTE KWAMBA MWOMBAJI ASIPEWE URAIA AMWANDIKIE SABABU HIZO:-

**KAMISHNA JENERALI WA UHAMIAJI,**
**S.L.P 512,**
**DAR ES SALAAM.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LAS CONSTRUCTION CO LTD. & STANBIC BANK TANZANIA LTD** inatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 349 BEH** aina ya Excavator Komatsu **PC 220 – 7** yenye Chassis namba **SAA6D1102E2A26368152**. Engine namba **255329.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/195283/2024**



### AFFIDAVIT OF ONE AND THE SAME PERSON

**CHANDE JUMA ABDALLAH** of P.O. Box ..............**DAR ES SALAAM** adult Muslim solemnly state as follows;

- That Iam the deponent herein hence conversant with the facts Iam about to depose.
- That I know by fact, I by the name **CHANDE JUMA ABDALLAH** appearing in my both certificate and National Identification Card refer to one and the same person as **JUMA CHANDE ABDALLAH** and **ANDREW JOHN LWANDA** appearing in my academic certificate and marriage certificates respectively.
- That the forenamed names of **CHANDE JUMA ABDALLAH, JUMA CHANDE ABDALLAH** and **ANDREW JOHN LWANDA** refer to one and the same person.
- That the above is the variations of the same name and should not be considered name changes.
- I execute this Affidavit to the truth of the foregoing facts and for whatever legal purpose that this Affidavit may serve.
- That all what is stated under paraghaph 1,2,3,4,5,6 are true to the best of my knowledge and beliefs.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**VAILETH NDEKIRWA NNKO** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 734 EPQ** AINA YA SINORAY. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/ARU/ARU/37453/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NDUGU MUSSA IBRAHIMU RAJABU** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA RUMION YENYE NAMBA ZA USAJILI T 805 DVT. KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ANAOMBWA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. AMEFIKA POLISI NA AMEPEWA LOSS REPORT. TAARIFA POLISI: **PHQ/TAN/TAN/9476/2024.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MWANZA**
**SHAURI LA MADAI NO. 18636/2024**
**Ref no. 20240801100018636**
**TATA AFRICA HOLDINGS..................MDAI**
**VERSUS**
**ALEXANDER PASTORY MNYETI.............MDAIWA**

**KWA: ALEXANDER PASTORY MNYETI**
**MWANZA**

**POPOTE ULIPO.**
**KUITWA SHAURINI**

ZINGATIA, Shauri tajwa hapo juu limepangwa kwa ajili ya kutajwa tarehe 07/10/2024 saa 09:30 Asubuhi. Mbele ya Mhe. B.M LEMA – PRM

Hivyo unatakiwa kuhudhuria Mahakamani hapa bila kukosa na kuwasilisha nyaraka zako zote na majibu ambayo mtaona ni vyema na muhimu katika kuthibitisha shauri hilo.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na kuwekwa mhuri wa Mahakama hii leo tarehe 17/09/2024.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI
MWANZA

### WILCO TANZANIA LIMITED

**[Company registration Number: 138842762]**
**(UNDER VOLUNTARY LIQUIDATION)**
**FINAL MEETING AND DISSOLUTION**
**(Made under Section 345 (1) & (2) of The Companies Act Cap 212 RE 2019)**

**NOTICE IS HEREBY GIVEN to the GENERAL PUBLIC that WILCO TANZANIA LIMITED** is undergoing Voluntary Liquidation and it has called for a Final Meeting and

Dissolution of the Company which is intended to be held at the REGISTERED OFFICES OF THE COMPANY MAK.AO VILLAGE, MAK.AO AREA, MWANHUZI, MEATU, SIMIYU, TANZANIA on the 15th _of _November_2024 at 1200 HOURS.

DA TED THIS _27th _DAY OF _September _ 2024

JOSEPH JACOB MBOGO
T/A ACME BUSINESS CONSULT
(LIQUIDATOR).
PLOT NO. 179, BLOCK 5, MBWENI JKT,
KINONDONI, DAR ES SALAAM.

### AMPATH PATHOLOGY DAR ES SALAAM LIMITED

**[Company registration Number: 99851]**
**PLOT NO.4 I, OSMAN TOWER, I sr FLOOR, ZANAKI STREET, ILALA CBD, DAR ES SALAAM, TANZANIA.**

### RE: NOTICE TO THE GENERAL PUBLIC OF RESOLUTION TO WIND UP VOLUNTARILY

In accordance with section 334(1) of the Companies Act, the company hereby notifies the general public that on 30th June 2024 it passed a special resolution to wind up the company voluntarily.

It was further resolved that Joseph Jacob Mbogo T/A ACME Business Consult of Plot No.179, Block 5, Mbweni JKT, Kinondoni, Dar es salaam be appointed as a liquidator of the Company.

Whoever has any claim against the company should notify the company within 14 days.

LOUIS BERNARD GERIC
COMPANY SECRETARY

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 06770 20701**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701***

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0677020701**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**Website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Israel, Iran zatunishiana misuli

**JERUSALEM,** Israel

MAMLAKA ya Israel imesema kitendo cha Iran kulishambulia taifa hilo ni uchokozi mkubwa ambao utatolewa majibu yanayostahili, huku Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UN) likifanya kikao cha dharura usiku wa kuamkia jana kujadili mzozo unaozidi kutanuka wa Mashariki ya Kati.

Aidha, wakati Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, akiapa kulipiza kisasi kutokana na mashambulizi hayo ya Iran, pia Iran nayo imejibu kupitia Rais Masoud Pezeshkian ikitishia kwamba itajibu vikali zaidi iwapo Israel itathubutu kufanya mashambulizi ya kulipiza kisasi.

Balozi wa Iran kwa Umoja wa Mataifa aliliambia baraza hilo kwamba madhumuni ya nchi yake kurusha dazeni ya makombora nchini Israel ni kwa ajili ya kuzuia taifa hilo kutoendelea na mashambulizi yake.

**Ilielezwa kuwa, vifo vya wanajeshi hao ndiyo mauaji ya kwanza ya wanajeshi wa Israel tangu ilipoanzisha mashambulizi ya ardhini huko Lebanon mapema wiki hii.**

Usiku wa kuamkia Jumatano, Iran ilivurumusha makombora ya masafa marefu yapatayo 180 kuelekea Israel ikisema ilikuwa ikiyalenga maeneo ya miundombinu ya kijeshi.

Israel ilisema asilimia kubwa ya makombora hayo yalinaswa na kuharibiwa na mfumo wa ulinzi wa anga kwa kusaidiwa na washirika wake kama Marekani, Uingereza na Ufaransa.

Lakini Tehran ilisisitiza kuwa makombora yake mengi yalilenga shabaha zao huku Mkuu wa Majeshi wa Iran Mohammad Bagheri, akiionya Israel kuwa isipojizuia, operesheni hiyo ya juzi usiku inaweza kujirudia.

Wakati huo huo, Balozi wa Israel katika Umoja huo wa Mataifa, Danny Danon alisema hatua hiyo ya Iran kuishambulia Israel ni kitendo kikubwa cha uchokozi na iwapo haitozuiliwa basi wimbi jengine la makombora halitoilenga tu Israel bali mataifa mengine pia.

Rais wa Marekani, Joe Biden alisema kuwa hatoiunga mkono Israel iwapo itashambulia miundombinu ya zana za nyuklia za Iran.

### HALI YA HATARI

Wakati hayo yakiendelea, ilielezwa kuwa Israel ambayo inapambana na wanamgambo katika ngome mbili, ikiwamo kundi la Hezbollah katika uvamizi wake wa ardhini nchini Lebanon pamoja na wanamgambo wa Hamas huko Gaza, imefanya mashambulizi yaliyosababisha vifo vya watu kadhaa juzi.

Pia ilielezwa kuwa vita hivyo vya Mashariki ya Kati vimesababisha miito ya usitishwaji mapigano kutolewa na viongozi na taasisi mbalimbali ikiwamo Umoja wa Mataifa na Ulaya.

Ilielezwa kuwa Naibu Kansela wa Ujerumani Robert Habeck, alisema hali ya Mashariki ya Kati ni hatari, akishauri kuwa kuna haja ya Ujerumani kushikamana na Israel huku akitoa wito wa diplomasia kutumika katika usitishwaji mapigano.

Jeshi la Israel lilitoa amri jana ya kuwataka watu waondoke katika maeneo kadhaa ya kusini mwa Beirut huko Lebanon, yaliyo na idadi kubwa ya watu, ikisema itayashambulia maeneo ya wanamgambo wa Hezbollah katika eneo hilo.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa Israel tayari imefanya mashambulizi katikati mwa mji huo mkuu wa Lebanon na kusababisha vifo vya watu sita. Huku Wizara ya Afya ya Lebanon ikisema watu wengine saba wamejeruhiwa katika shambulizi hilo la usiku wa kuamkia jana.

Vile vile, ilielezwa kuwa Jeshi la Israel kwa upande wake limepata pigo pia kwani limethibitisha kwamba wanajeshi nane wameuawa, huku saba wakijeruhiwa vibaya kusini mwa Lebanon kutokana na mashambulizi ya wanamgambo wa Hezbollah.

Ilielezwa kuwa, vifo vya wanajeshi hao ndiyo mauaji ya kwanza ya wanajeshi wa Israel tangu ilipoanzisha mashambulizi ya ardhini huko Lebanon mapema wiki hii.

Wakati hayo yakiendelea, ilielezwa kuwa maelfu ya raia wa Lebanon wanaendelea kumiminika nchini Syria wakiyakimbia mashambulizi ya Israel kusini mwa Lebanon.

Kikosi cha waandishi wa habari wa shirika la habari la Associated Press, kilisema kimeshuhudia mamia ya watu wakikusanyika katika kivuko cha mpakani cha Jousieh, ambacho ni mojawapo ya njia za kuingia Syria. **APE/AFP/DW**

# Wabunge wahofia usalama wao

**NAIROBI,** Kenya

BAADHI ya wabunge nchini Kenya wana wasiwasi kuhusu usalama wao katika kipindi cha kuanza kujadili hoja ya kumtimua Makamu wa Rais Rigathi Gachagua baada ya kuwasilishwa hoja ya kutokuwa na imani nae.

Ilielezwa kuwa wabunge hao walimsihi Spika wa Bunge, Moses Wetang'ulah kuingilia kati kwa kuagiza mamlaka husika kuimarisha usalama wao na wa Rais William Ruto wakati wa shughuli hiyo.

Mbunge wa Kikuyu na kiongozi wa walio wengi Kimani Ichung'wah alidai kuwa wabunge walindwe ipasavyo sio tu katika maeneo ya bunge bali hata majumbani mwao.

Pia wabunge hao walielezea wasiwasi wao kuhusu usalama wao baada ya kupewa notisi ya hoja ya kumshtaki Makamu wa Rais nchini humo Rigathi Gachagua.

Ilibainishwa kuwa jumla ya wabunge 291 walitia saini kuunga mkono hoja hiyo. Na kwamba Mbunge wa Suna Mashariki, Junet Mohamed, alipothamini ukubwa wa suala hilo mbele ya Bunge, alielezea wasiwasi wake kuhusu usalama wa wabunge wanaoshiriki katika kesi dhidi ya Gachagua.

Alidokeza kwamba wale wanaounga mkono hoja hiyo wanaweza kutishwa au kuwekwa njiani au hata kukabiliwa na hali mbaya ya kiusalama katika jitihada za watu wasiojulikana ili kukandamiza kesi hiyo.

Mbunge huyo alirejelea matukio ya Capitol Hill mnamo 2021 wakati wafuasi wa rais wa zamani wa Merika Donald Trump walipovamia Bunge la Congress, na kuwafanya wabunge waliojawa na hofu kujificha.

Mbunge wa Daadab, Farah Maalim alishiriki katika wasiwasi huo huo, akiomba usalama zaidi sio tu kwa wabunge hao bali pia kwa Rais William Ruto.

"Mimi pia naungana na wenzangu katika hili. Lakini nataka tu kuzungumzia suala muhimu zaidi, sio tu kulinda maisha ya wabunge 291 ambao wametia saini huko. Ni lazima tulinde mfumo. IG lazima alinde maisha yetu.

"Rais mzembe, jambazi yeyote mzembe anaweza kuamua kubadili historia...kama Mungu angezuia jambo lolote lisitokee kwa rais wetu, basi tunalo jambo kubwa zaidi la kuhangaikia rais wetu hadi hoja hii iishe," alisema Maalim.

### KUHUSU RUTO

Wakati sakata hilo likiendelea ilielezwa kuwa Rais Ruto aliendelea kujitenga kabisa na matatizo yanayomkabili naibu wake Gachagua, ambaye kazi yake sasa imo hatarini.

Ilielezwa kuwa ukimya mkubwa wa Rais Ruto kuhusu mchakato unaomkabili naibu wake umesababisha wengi kufikia hitimisho kwamba anaunga mkono hoja hiyo.

Ilielezwa kuwa Rais Ruto alikuwa ndani ya eneo la Ikulu wakati ilani ya kumwondoa Gachagua ikiwasilishwa rasmi katika Bunge la Kitaifa Oktoba 1, mwaka huu.

Ilielezwa kuwa Waziri wa Kazi na Ulinzi wa Jamii Alfred Mutua, ambaye ni wa chini ya Rais Ruto kwenye Baraza la Mawaziri, pia aliunga mkono hoja hiyo ya kumwondoa Gachagua.

Wakati wa kuwasilisha ilani ya hoja hiyo Jumanne, Mbunge wa Kibwezi Mwengi Mutuse, aliyekuwa mwendeshaji wa hoja hiyo, aliweka madai kadhaa juu ya jina la Gachagua, akiahidi kutoa ushahidi wa kila moja katika jitihada zake za kuwashawishi wenzake kumwondoa naibu wa rais. **KTN**



Wanamgambo wa Hezbollah ambao wanapambana na Israel katika mpaka wa Lebanon. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA QUEENS YAELEZA VIBALI VIMEWAANGUSHA

Na Adam Fungamwango

KOCHA Msaidizi wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi', amesema sababu kubwa iliyopelekea timu yao kupoteza mchezo wa Ngao ya Jamii dhidi ya Yanga Princess ni kuchelewa kupatikana kwa vibali vya kazi kwa wachezaji wake wa kigeni.

Simba Queens ilikubali kichapo cha penalti 4-3 dhidi ya watani zao wa jadi, Yanga Princess, baada ya kumaliza sare ya bao 1-1 katika dakika 90 za kawaida, mchezo uliofanyika kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam juzi.

Mgosi alisema kiufundi walikuwa vizuri, lakini tatizo kubwa lilikuwa ni ucheleweshwaji wa vibali hali iliyolazimika wapangue kikosi cha kwanza ambacho tayari kilikuwa kimepangwa.

"Kilichonifelisha ni ucheleshwaji wa vibali vya wachezaji wangu wa kigeni tu. Niwapongeze wachezaji wangu wamecheza kwenye plani tuliyopanga, ila nadhani mambo ya vibali yameniangusha, kulikuwa na ucheleshwaji wa kupatikana na vibali, dakika tano kabla ya mchezo kuanza tukaambiwa baadhi ya wachezaji hawakuwa na leseni kutokana na kutokamilika kwa vibali, imewachanganya sana wachezaji wangu, ndiyo maana tukaruhusu bao mapema tu, lakini tulisawazisha, tukaenda kwenye penalti tukashindwa, nadhani bahati ilikuwa kwa Yanga Princess safari hii," Mgosi alisema.

Simba Queens haikuanza na wachezaji wake tegemeo kama Vivian Corazone, Precious Christoper, Elizabeth Wambui na wengine kitu ambacho kiliwashangaza wengi, na waliingia dakika chache baada ya mapumziko kutokana na taratibu kukamilika.

**Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Edna Lema, aliwapongeza wachezaji wake kwa ushindi, lakini hakupendezwa na wapinzani wao kutokamilika.**

"Sikupendezwa sana na wachezaji wao kucheleshwa vibali kwa sababu nilitaka wawe kamili ili kuwe na ushindani mkali, tuwafunge wakiwa wamekamilika kusiwe na visingizio, lakini ndiyo hivyo imetokea.

Timu yangu bado ni mpya, lakini wachezaji wamejitahidi sana, mapungufu yaliyojitokeza tutayafanyia kazi, niwapongeze Simba Queens, ni timu nzuri na wameleta upinzani mkali sana," alisema kocha huyo.

Kwa ushindi huo, Yanga Princess imetinga fainali ya Ngao ya Jamii na kesho itacheza fainali dhidi ya JKT Queens iliyoifumua Ceasiaa Queens mabao 7-0 katika mchezo wa nusu fainali ya kwanza ya michuano hiyo.

# Michuano ya CDF kuanza leo

Na Shufaa Lyimo

SHINDANO la Mkuu wa Majeshi (CDF Trophy 2024), linatarajiwa kufanyika kuanzia leo hadi Oktoba 6, mwaka huu kwenye Klabu ya Jeshi ya Lugalo jijini Dar es Salaam, imeelezwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Klabu ya Lugalo, Brigedia Jenerali Mstaafu, Michael Luwongo, alisema lengo la shindano hilo ni kumwenzi Mkuu wa Majeshi ambaye pia ni mlenzi wa klabu, Jenerali, Jacob Mkunda.

"Lengo ni kumwenzi Mkuu wa Majeshi kwa kuazimisha kuzaliwa kwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), ambalo huazimishwa kila ifikapo Septemba Mosi ya kila mwaka, " alisema Luwongo.

Alisema mpaka sasa zaidi ya washiriki 100 kutoka klabu mbalimbali nchini wamethibitisha kushiriki na anawaomba Watanzania wajitokeze kwa wingi kushuhudia vipaji vitakavyoonyeshwa katika mashindano hayo.

"Kwa sasa maendeleo ni mazuri kwa sababu klabu nyingi zimethibitisha kushiriki shindano hilo ambalo naamini litakuwa na mvuto wa aina yake," Luwongo aliongeza.

Mwenyekiti huyo alisema mshindi wa kwanza atapata zawadi ya Sh. milioni nne na zawadi hiyo iliyotangazwa itaongeza hamasa kwa wachezaji.

"Lengo letu ni kuona vipaji vinaendelea kukua na mchezo unapata mashabiki wengi zaidi," alisema.



Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Soka la Ufukweni wakifanya mazoezi ili kujiandaa na Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (BAFCON 2024), zitakazofanyika hivi karibuni nchini Misri. **PICHA: TFF**

# KVZ yataka pointi tisa za Ligi Oktoba

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

MAAFANDE wa KVZ FC wamesema wamejipanga kupambana ili kupata ushindi katika mechi zao tatu za Ligi Kuu Zanzibar zitakazochezwa ndani ya mwezi huu.

Katika michezo yake minne ambayo KVZ imecheza tayari wamepata sare tatu na ushindi mmoja na kwenye msimamo wa ligi hiyo wako nafasi ya saba baada ya kujikusanyia pointi sita kibindoni.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa habari wa timu hiyo, Abduljalili Mohamed, alisema wamepanga kuanza kuvuna pointi katika mchezo wao wa leo dhidi ya Zimamoto SC ili kufikia malengo yao.

Mohamed alisema anafahamu hakuna mechi rahisi katika ligi hiyo inayodhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), lakini wachezaji wake wamedhamiria kuondoka na ushindi kwenye mechi zote tatu zinazofuata.

Alisema kikosi chao hivi sasa kimetimia baada ya wachezaji wao nane wa kikosi cha kwanza kurejea mazoezini baada ya kurejea kutoka kwenye mashindano ya majeshi.

Alisema tayari wachezaji wote wameungana na kupata mazoezi ya pamoja kwa kufuata mpango wa mazoezi anaoendelea chini ya kocha mkuu wa timu hiyo.

Alisema kupitia mapumziko marefu karibu ya wiki mbili kwa timu hiyo wanarejea uwanjani kivingine hasa katika kuhakikisha kutimiza mpango wao.

"Mwezi huu wa Oktoba tumeuita Mwezi wa Kufosi, michezo mitatu tutakayoicheza mwezi huu tunataka kuhakikisha tunashinda yote kwa kuanzia na mechi yetu dhidi ya Zimamoto SC tutakayocheza kesho (leo)," alisema.

Aliongeza huku ligi hiyo ikiwa imeingia katika mzunguko wa tano, ligi hiyo ni ngumu na hakuna timu yenye uhakika wa kupata mechi yenye mteremko.

"Ligi ni ngumu na kila siku timu zinaimarika, kila timu imejipanga kupata alama za mapema ili kujiweka katika nafasi salama," aliongeza.

Kiongozi huyo amewaomba mashabiki wa timu hiyo kujitokeza kwa wingi uwanjani ili kuipa hamasa timu yao na kuwa sehemu ya kufanikisha mipango na malengo.

**Ligi ni ngumu na kila siku timu zinaimarika, kila timu imejipanga kupata alama za mapema ili kujiweka katika nafasi salama.**

## ZISIKUPITE

### CHELSEA, WEST HAM VITANI

CHELSEA na West Ham ni baadhi ya klabu zinazomfuatilia kwa karibu mshambuliaji wa Aston Villa na Timu ya Taifa ya Colombia, Jhon Duran, mwenye umri wa miaka 20. ***(Give Me Sport)***

### FOREST KUMUUZA MURILLO

KLABU ya Nottingham Forest itamuuza Murillo bila kutaka, ikiwa watapokea ada kubwa kwa beki huyo wa kati wa Brazil mwenye umri wa miaka 22, ambaye amekuwa akihusishwa na Barcelona na Real Madrid. ***(Football Insider)***

### MUSIALA AITAMANI EPL

WINGA wa Ujerumani, Jamal Musiala, mwenye umri wa miaka 21, ambaye mkataba wake na Bayern Munich utatamatika ifikapo mwaka 2026, alisema alikuwa wazi kwa kila kitu lakini ana furaha sana huenda siku moja akacheza Ligi Kuu England. ***(Guardian)***

### BAENA ATAJWA NEWCASTLE

WINGA wa Villarreal ambaye ni raia wa Hispania, Alex Baena, mwenye umri wa miaka 23, amewavutia maskauti wa Aston Villa na Newcastle United msimu huu. ***(Caught Offside)***

### BAYERN WAITAMBIA UNITED

WAKUU wa Bayern Munich wanaamini walimsajili nyota wa pauni milioni 100 kwa kiasi cha nusu dau pale waliiposhinda Manchester United kwenye usajili wa pauni milioni 50 wa winga wa Ufaransa, Michael Olise, 22, kutoka Crystal Palace. ***(Mirror)***

### POTTER KUMRITHI MARTIN

KLABU ya Southampton inaweza kumgeukia kocha wa zamani wa Chelsea na Brighton, Graham Potter, iwapo wataamua kumfukuza, Russell Martin. ***(Football Insider)***

### DYCHE: SIONDOKI EVERTON

SEAN Dyche ameelezea wazi nia yake ya kutaka kubaki kama kocha wa Everton baada ya klabu kununuliwa na kuwaongoza katika uwanja wao mpya. ***(Telegraph)***

### EZE AFURAHIA CRYSTAL

WINGA wa England, Eberechi Eze, ameridhika na nafasi yake huko Crystal Palace, ambao walishangazwa kutopokea ofa kutoka kwa klabu za Ligi Kuu England wakati wa msimu wa joto. ***(Mirror)***

### WILSON NJIA MOJA

KLABU ya Newcastle United iko tayari kumruhusu mshambuliaji wa England, Callum Wilson, 32, kuondoka bila malipo msimu ujao iwapo hawatapata mbadala wake ifikapo Januari. (***Give me Sport)***

### YAZICI MAMBO YAMEIVA

MSHAMBULIAJI wa Uturuki, Yusuf Yazici, 27, anatazamiwa kusaini mkataba wa miaka mitatu na klabu ya Ugiriki ya Olympiakos baada ya kuamua kuondoka Lille ya Ufaransa. ***(Fabrizio Romano)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ANCELOTTI: MADRID TULISTAHILI KICHAPO

### Kocha huyo adai haukuwa 'usiku mzuri' kwao na...

**MONACO,** Ufaransa

CARLO Ancelotti amesema ukosoaji wa kichapo cha bao 1-0 cha Real Madrid katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kutoka kwa Lille ulikuwa "wa haki" na timu "haipaswi kutafuta visingizio" baada ya kuhangaika dhidi ya timu hiyo ya Ligue 1.

**Penati ya Jonathan David kabla ya kipindi cha mapumziko kwa mpira wa mkono wa Eduardo Camavinga lilikuwa bao pekee katika mchezo huo uliochezwa juzi usiku.**

Endrick na Vinícius Júnior walipata nafasi za kipindi cha kwanza kwa Madrid, huku Jude Bellingham, Antonio Rüdiger na Arda Güler wote wakikaribia kufunga.

"Mpinzani alicheza vizuri zaidi, na alistahili kushinda," alisema Ancelotti katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi.

"Katika suala la pambano, nguvu, uthibiti. Tunapaswa kujifunza kile cha kuboresha, ambacho ni dhahiri kabisa, sio ngumu sana.

"Leo (juzi) kila kitu kilikuwa kibaya sana. Tulikuwa wabaya na mpira. Ilikuwa ngumu kwetu kushinda mpira. Ilikuwa ngumu kwetu kuvuka. Tulihitaji kuwa wakali zaidi. "Hisia ilikuwa ngumu kwetu kuunda. Umiliki wetu wa mpira ulikuwa wa pole pole sana, na mawazo machache. Tuna washambuliaji ambao wanahitaji kucheza wima zaidi. Ikiwa ni ngumu kwao kudhibiti mpira, na utapata.

Matokeo hayo yanaifanya Madrid kusalia na pointi tatu katika michezo miwili ya awamu ya makundi ya Ligi ya Mabingwa hadi sasa, na katika nafasi ya 17 kwenye jedwali la timu 36.

"Huzuni inatokana na hisia za timu, haukuwa mchezo mzuri," aliongeza Ancelotti.

"Haukuwa usiku mzuri, tusitafute visingizio, lazima tuboreshe.

"Mimi ni mkweli sana. Kukosolewa kwa mchezo huu ni sawa, sawa, lazima tukubali."

Jambo moja chanya kwa Madrid, ulikuwa mwanzo wa Ligi ya Mabingwa kwa Endrick, baada ya fowadi huyo kufunga kama mchezaji wa akiba dhidi ya Stuttgart kwenye mechi yake ya kwanza ya shindano hilo.

# MARTÍNEZ: SHANGWE VILLA PARK ZILINIUMIZA MASIKIO



**BIRMINGHAM,** England

GOLIKIPA wa Aston Villa, Emiliano Martínez, amesema kelele za umati wa mashabiki zilikuwa kubwa zaidi kuwahi kusikia akiwa Villa Park baada ya kuisaidia timu yake kuifunga Bayern Munich bao 1-0 katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya juzi usiku.

Bao la Jhon Duran dakika ya 79 lilitosha kuipa Villa ushindi wa kukumbukwa dhidi ya Bayern Munich ya Vincent Company ikiwa ni mechi ya kwanza ya wenyeji kwenye ngazi ya juu ya michuano ya Ulaya kwenye Uwanja wa Villa Park katika kipindi cha miaka 41.

Bayern Munich walimiliki mpira kwa wingi na walipata nafasi ya kusawazisha mwishoni mwa mechi, lakini Martinez aliokoa kwa ustadi mpira wa kichwa uliopigwa na Harry Kane. Na baada ya mechi, mshindi huyo wa Kombe la Dunia na Argentina alitoa pongezi kwa mashabiki na kujitolea ushindi wao.

"Hii ndiyo Villa Park yenye sauti kubwa zaidi ambayo nimeisikia tangu nilipojiunga na klabu, hilo ni la uhakika," alisema Martinez.

"Ilikuwa inaumiza masikio yangu wakati fulani. Ninapenda kucheza hapa. Nawapenda mashabiki. Huu ni ushindi kwao."

"Hakuna ukomo kwangu, nataka kuendelea kuimarika," aliongeza mlinda mlango huyo wa timu ya taifa ya Argentina.

"Nina nia ya kuendelea kusonga mbele, kuwa bora zaidi, kushinda kila kitu nikiwa na Aston Villa, na timu ya taifa ya Argentina pia, na ninajaribu kuionesha kila wiki.

Mashambulizi bora yaliyookolewa na Martinez yalihifadhi alama tatu, walikuwa na bao la ajabu la Duran kushukuru kwa ushindi maarufu.

Bao hilo lilipatikana wakati mpira mrefu wa Pau Torres ulipogawanya safu ya ulinzi ya Bayern na Duran akapiga shuti la kwanza kutoka umbali wa yadi 30 lililopita juu ya kichwa cha kipa Manuer Neuer.

# Messi aipa Miami taji la kwanza MLS



**OHIO,** Marekani

LIONEL Messi amesema Inter Miami CF imekamilisha lengo lake la kwanza la msimu wa MLS wa 2024 baada ya kutwaa Ngao ya Mashabiki kwa ushindi wa magoli 3-2 dhidi ya Columbus Crew hapo juzi usiku kwenye Uwanja wa Lower.com mjini Ohio.

"Nina furaha," alisema Messi katika mahojiano baada ya mchezo na Apple TV.

"Nimefurahi tulifanya hivyo. Mwanzoni mwa mwaka tulijua hili ni kundi la kupigania. Tulichukua jukumu tangu mwanzo, tulikuwa na wachezaji wa kufanya hivi. Nina furaha kupata lengo la kwanza, na tunafikiria ijayo."

Messi alifunga mabao mawili na Luis Suárez akaongeza lingine huku Miami wakisawazisha baada ya Rudy Camacho wa timu hiyo kutolewa nje kwa kadi nyekundu dakika ya 63.

Kipa wa Miami, Drake Callender, aliokoa mkwaju wa penalti kutoka kwa Cucho Hernández dakika ya 84.

The Herons walipata kombe hilo wakiwa na pointi 68 katika michezo 32, na kushinda taji lao la kwanza kwenye MLS tangu ilipoanza kuchezea mwaka 2020.


Inter Miami ilitwaa taji la kwanza la Kombe la Ligi 2023 lakini hapo awali walikuwa hawajashinda chochote katika MLS.

Timu hiyo ilipata ongezeko la hali ya hewa mnamo 2024 kutokana na mchango wa Messi na Suárez katika misimu yao ya kwanza kamili na timu. Kwa pamoja, washambuliaji hao wamechangia mabao 35 kati ya 72 ya timu hiyo katika mechi 31.

# Zubimendi hajutii kuikataa Liverpool

**MADRID,** Hispania

KIUNGO wa kati wa Real Sociedad na Hispania, Martín Zubimendi, amesema hajutii uamuzi wake wa kukataa kuhamia Liverpool msimu wa joto.



Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 alikuwa chaguo bora zaidi la Liverpool katika safu ya kiungo ya ulinzi lakini licha ya harakati zao za muda mrefu, Zubimendi aliamua kubaki katika klabu ambayo ametumia tangu utoto.

La Real wamevumilia mwanzo mgumu katika LaLiga msimu huu wakiwa wameshinda mara mbili pekee katika mechi nane za mwanzo.

"Kwa kweli sijutii, siwezi kufikiria hivyo baada ya mechi nne au tano mwanzoni mwa msimu. Nilifanya uamuzi wangu kutoka ndani ya moyo niliona ni jambo bora kufanya, matokeo hayafanyi hivyo," naona uwezo katika timu hii, lazima utuangalie tukifanya mazoezi ninafuraha kuwa na msimu mzuri," alisema.

"Mwisho kama katika kila dirisha la uhamisho, mambo huwa yanatokea. Msimu huu ilikuwa zamu yangu. Haya ni mambo ambayo hutokea na unapaswa kukabiliana navyo kwa njia bora zaidi.

"Ni kweli nilikuwa sina raha na kila kitu, haswa kelele, lakini mwisho nilijitenga na kufanya uamuzi ambao nilifikiri ndio sahihi."

Wasifu wa Zubimendi uliongezeka majira ya kiangazi baada ya kuichezea Hispania kwenye michuano ya Euro 2024.

## Transit, Geita Gold kibaruani

**Na Adam Fungamwango**

RAUNDI ya tatu ya Ligi ya Championship inaendelea leo Maafande wa Transit Camp kuwakaribisha Geita Gold, mechi itakayochezwa kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Dar es Salaam.

Maafande hao hawajashinda mchezo wowote kati michezo miwili iliyocheza Geita Gold nayo ikiwa haijashinda, lakini imetoa sare michezo yote miwili.

African Sports itakuwa kwenye Uwanja wa Jamhuri Morogoro ikiikaribisha Songea United, ambayo imeonekana kuwa tishio kwenye ligi hiyo.

Vigogo hao wa Tanga, Africans Sports nao hawajashinda mchezo wowote, ikitoka sare moja na kupoteza mmoja, inacheza na Songea United, ambayo imeshinda michezo yake yote miwili na kushika nafasi ya pili ya msimamo, ikiwa na pointi sita.

Mechi nyingine itakayopigwa leo ni kati ya Kiluvya FC ya Pwani, ambayo itashuka Uwanja wa Mabatini, Mlandizi kucheza dhidi ya Polisi Tanzania.

Kiluvya, ambayo ni mara ya kwanza kucheza Ligi ya Championship ikitoka 'first league', imepoteza michezo yote miwili ambayo imeshacheza sawa na Polisi Tanzania iliyoshuka kutoka Ligi Kuu Bara msimu uliopita.

## Yanga yasaka

INATOKA UK. 24

mara kwa mara kutua Jangwani.

"Mahesabu ya Yanga ni huyu ndiyo atakuwa mchezaji wa kwanza kusajiliwa, na kama kuna wengine basi watafuata," alisema mtoa taarifa.

Habari zaidi zinasema Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, ameonekana kuridhishwa na viungo washambuliaji, mastraika na mawinga alionao, lakini bado haridhishwi na eneo la kiungo mkabaji. Kwa sababu hiyo, huenda mchezaji hiyo akasajiliwa kuchukua nafasi ya Jean Baleke, ambaye ameonekana hana namba ya kudumu katika kikosi cha kwanza cha timu hiyo.

Taarifa zaidi zinadai huenda Baleke akapelekwa kwa mkopo Singida Black Stars ili nafasi yake ichukuliwe na kiungo huyo mpya.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, amesema kwa sasa si wakati wa usajili, hivyo hawezi kueleza chochote kuhusu mchakato huo na badala yake wako kwenye operesheni ya kuhakikisha wanapanda kileleni kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tuko kwenye operesheni ya kuisaka nafasi ya kwanza katika msimamo wa Ligi Kuu, nafasi yetu pendwa ni namba moja, hatuna chochote tutakachoongea au kuwaza zaidi ya kwanza tukae kwenye sehemu tulioizoea, namba moja," alisema Kamwe.

# SIMBA QUEENS, YANGA DIMBANI TENA NOVEMBA

**Na Mwandishi Wetu**

WATANI wa jadi nchini, Simba Queens na Yanga Princess watakutana katika mechi ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania itakayochezwa Novemba 13, mwaka huu kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

**Timu hizo zitarudiana katika mchezo wa mzunguko wa pili utakaofanyika Machi 4, mwakani kwenye uwanja huo huo.**

Yanga Princess itashuka dimbani katika mechi hiyo ikiwa na kumbukumbu ya kupata ushindi wa kwanza wa penalti 4-3 ambao wameupata kwenye mechi ya hatua ya nusu fainali ya pili ya michuano ya Ngao ya Jamii iliyochezwa juzi jijini.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), mabingwa watetezi, Simba Queens watafungua pazia la msimu mpya wa 2024/2025 kwa kuwakaribisha Mlandizi Queens mechi itakayochezwa Oktoba 9, mwaka huu kwenye Uwanja wa KMC Complex wakati Yanga Princess itaanzia ugenini dhidi ya Bunda Queens siku hiyo hiyo.

Alliance Girls watakuwa nyumbani kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza kuwakaribisha JKT Queens wakati Gets Program ya Dodoma itawafuata Mashujaa Queens (zamani Amani Queens), kwenye Uwanja wa Isamuhyo, Dar es Salaam na Fountain Gate Princess itakuwa na kibarua dhidi ya Ceasiaa kutoka mkoani Iringa.

Ligi hiyo inayoshirikisha timu 10 imepangwa kumalizika Mei 6, mwakani kwa Fountain Gate Princess kuwavaa Mlandizi Queeen, Mashujaa Queens yenyewe itapambana na Bunda Queens huku JKT Queens itawafuata Gets Program, Alliance Girls itapapatuana na Simba Queens huku Yanga Princess ikiwaalika Ceasiaa kwenye Uwanja wa KMC Complex.

Simba Queens ilitwaa ubingwa wa ligi hiyo msimu uliopita bila kufungwa, pia ikishinda Ngao ya Jamii kwa kuwafunga JKT Queens kwenye mchezo wa fainali.

Bingwa wa ligi hiyo atapata nafasi ya kuiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), yanayofanyika kila mwaka.

Wakati huo huo, Mwenyekiti wa Chama cha Mpira wa Miguu cha Wanawake Tanzania (TWFA), Somoe Ng'itu, amewapongeza wadau wa soka waliojitokeza katika mechi za hatua ya nusu fainali ya Ngao ya Jamii zilizofanyika juzi.

"Tunawashukuru kwa kujitokeza kushangilia timu zao, tunawaahidi msimu mpya utakuwa na ushindani zaidi, kwa sababu kila timu imejipanga na imejiandaa vyema," Somoe alisema.




Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Saadi Mtambule (kulia), akizungumza katika Semina ya Usalama iliyoandaliwa na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT) yenye lengo la kutoa mafunzo ya kuendeleza michezo hiyo ili kukusanya kodi wilayani humo. Kushoto ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa GBT, James Mbalwe. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids

## Simba yaitisha Coastal Union

INATOKA UK. 24

mani wa timu hiyo.

Simba haijafungwa mchezo wowote wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union tangu Ligi Kuu msimu wa 2019/2020, ikiwa imecheza michezo 12, ikishinda michezo 10 na sare mbili.

Msimu huu Wekundu wa Msimbazi wamecheza michezo minne, wameshinda yote, ikikusanya pointi 12 na mabao 10 kibindoni huku haijaruhusu nyavu zake kutikiswa wakati Coastal Union walioshuka dimbani mara sita, wameshinda mechi moja, sare moja na kupoteza minne, ikiwa na pointi nne.

Wakati huo huo, Singida Black Stars imetamba itaondoka na ushindi katika mechi yake ya leo dhidi ya Mashujaa FC ingawa wanaamini mchezo huo utakuwa mgumu na wenye upinzani.

Kocha Msaidizi wa Singida Black Stars, Dennis Kitambi, alisema jana anatambua ugumu wa mchezo huo na kuahidi licha ya kucheza ugenini lakini watapata ushindi.

"Tunafahamu Mashujaa ni timu ngumu ambayo hairuhusu magoli kirahisi, nimeandaa vizuri wachezaji wangu kuhakikisha tunapata matokeo mazuri katika mchezo wetu huo," alisema Kitambi.

Mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini Mbeya itakuwa ni kati ya wenyeji KenGold dhidi ya JKT Tanzania.

# Michezo

Ijumaa Oktoba 4, 2024

Nipashe




Messi aipa Miami taji

UKURASA 22

PISHA NIPITE...



Straika wa Yanga Princess, Adebisi (kulia), akijiandaa kumtoka beki wa kati wa Simba Queens, Fatma Issa 'Fetty Densa' katika mechi ya nusu fainali ya Ngao ya Jamii ya Wanawake iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam juzi. Yanga Princess ilishinda kwa penalti 4-3. **PICHA: TFF**

## Yanga yasaka kiungo mpya

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya Simba kumsajili winga, Elie Mpanzu, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga nao wako katika mchakato wa kunasa saini ya kiungo mkabaji mpya, Charve Onoya, kutoka AS Maniema ya nchini humo.

Habari kutoka ndani ya Yanga zinasema mchezaji huyo ni mmoja ya watakaovaa uzi wa kijani na njano kipindi cha dirisha dogo la usajili litakalofunguliwa Desemba, mwaka huu na Januari, mwakani.

Chanzo chetu kilisema Yanga inataka huduma ya mchezaji hiyo kwa ajili ya kuimarisha eneo lao la kiungo, ambalo kwa sasa linaongozwa na Mganda Khalid Aucho na Aziz Andambwile.

Kiungo huyo nusura ajiunge na Yanga mwanzoni mwa msimu huu, lakini dili lilifeli, na safari hii mabosi wa klabu hiyo wamerejea kwa nguvu zote.

"Kwa sasa tegemeo ni Aucho, na anaonekana amechoka kutokana na kucheza michezo mingi, anahitaji msaidizi, Mudathir yeye anapewa kazi ya kwenda kushambulia mianya inayoachwa na wapinzani, mara chache anakuja kumsaidia.

Andambwile bado hana uzoefu, tuna michuano mingi migumu ya kimataifa, kwa hiyo lazina tupate kiungo mkabaji mzuri na mwenye uzoefu, tumeangukia kwa huyo jamaa Mkongomani," kilisema chanzo kutoka Yanga.

Chanzo hicho kiliongeza upatikanaji wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, umechangiwa zaidi ya kiungo mshambuliaji, Maxi Nzengeli ambaye anatajwa ni rafiki yake na amekuwa akimshawishi

INAENDELEA UK. 23

# Simba yaitisha Coastal Union

**Somoe Ng'itu na Adam Fungamwango**

## Fadlu asema amepata 'dawa', Wagosi wa Kaya watamba...

USHINDI mnono ndio matarajio ya Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, kuelekea mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union kutoka jijini Tanga utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

**Hata hivyo Kaimu Kocha Mkuu wa Coastal Union, Joseph Lazaro, amesema endapo watatumia udhaifu wa Simba, timu hiyo inafungika.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Fadlu alisema ameendelea kulifanyia kazi suala la kukosa nafasi za wazi kwa wachezaji wake, na anaamini wakitumia vizuri nafasi watakazo zitengeneza watapata ushindi mnono katika mechi hiyo itakayochezwa kuanzia saa 10:15 jioni.

"Nimelifanyia kazi suala ya kukosa nafasi, utakumbuka Leonel Ateba katika mchezo uliopita dhidi ya Dodoma Jiji alikosa mabao kama mawili akiwa ndani ya boksi, ni kweli katika mchezo wa mpira wa miguu huwezi kupata kila nafasi na huwezi kushinda mabao matatu au manne kila mchezo, lakini tutajitahidi tuwe tunatumia vizuri nafasi zinazopatikana," Fadlu, raia wa Afrika Kusini alisema.

Kocha huyo alisema ana wasiwasi wapinzani wao wanaweza kuingia na mfumo wa kupaki basi, hivyo tayari ametengeneza mpango mkakati wa kuhakikisha wanafungua mianya.

"Kama wapinzani wetu watakuja na mfumo wa kuzuia, basi tunajaribu kuwalazimisha kuachia mianya, lakini pia na sisi inabidi tuwe makini kwa sababu wapinzani wetu ni wazuri wanapokuwa na mpira.

Tunaiheshimu Coastal Union, tuliiona ikicheza kwenye mechi za Ngao ya Jamii, ikacheza michezo miwili ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho, kwa sasa imeonekana kuimarika kwa hiyo itakuwa na mechi ngumu, lakini tumejipanga kutimiza malengo yetu," alisema Fadlu.

Naye Lazaro aliliambia gazeti hili katika mchezo huo, kila timu inahitaji kupata matokeo chanya, lakini wao wanayahitaji zaidi.

Lazaro alisema anawafahamu vyema wapinzani wao na wamejiandaa kuwadhibiti ili kuhakikisha wanavuna pointi katika mchezo huo.

"Kila mtu anahitaji matokeo, lakini sisi tunahitaji zaidi kwa sababu nafasi tuliyopo si rafiki, tunajua tunacheza na timu gani, wakoje, tucheze nao vipi, kwa sababu ni timu ambayo mchezaji mmoja tu anaweza kuamua matokeo, na wanao (wachezaji), kama watatu hivi," Lazaro alisema.

Aliongeza Simba pia ina udhaifu wake na endapo watautumia vyema, wanauwezo wa kupata ushindi.

"Pamoja na mazuri, wao pia wana udhaifu na wanafungika," alimaliza beki wa kushoto wa za-

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >